

MADA: "UKUZAJI WA KISWAHILI"

Na: MUKHWANA, AYUB

"Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya "Bachelor of Arts" katika Chuo Kikuu cha Nairobi."

1988




UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

EAST AFRICANA COLLECTION


UNGAMO

"Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya Shahada katika Chuo Kikuu Kingine chochote"



Mukhwana Ayub
(Mtahiniwa)

"Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii wa Chuo Kikuu"



Profesa Karega Mutahi



Dakta Jay Kitsao

YALIYOMO

Kurasa

Ungamo.....	i
Yaliyomo.....	ii
Shukrani.....	v

SURA YA KWANZA

1.0	Utangulizi wa Utafiti	1
1.1	Sababu za kuchagua somo hili.....	1
1.2	Lengo la tasnifu.....	2
1.3	Upeo na mipaka ya tasnifu.....	3
1.4	Tatizo linalotafitiwa.....	4
1.5	Yaliyoandikwa kuhusu somo hili.....	4
1.6	Njia za utafiti.....	5
1.7	Hitimisho la mwongozo.....	7
1.8	Tanbihi.....	8

SURA YA PILI

2.0	Usanifishaji wa Kiswahili.....	9
2.1	Utangulizi.....	9
2.2	Masiala yaliyosababisha usani- fishaji wa Kiswahili.....	10
2.3	Usanifishaji wa Kiswahili na 'Kasoro Zake'.....	15
2.4	Manufaa ya usanifishaji wa Kiswahili.....	21
2.5	Hitimisho.....	26
2.6	Tanbihi.....	29

SURA YA TATU

3.0	Ukuzaji wa Kiswahili baada ya Uhuru.....	31
3.1	Utangulizi.....	31
3.2	Vyombo vya habari na ukuzaji wa Kiswahili.....	32
3.21	Magazeti.....	32
3.22	Redio na Televisheni.....	36
3.3	Waandishi wa Vitabu.....	36
3.31	Vitabu vya Fasihi.....	39
3.32	Vitabu vya Sarufi.....	40
3.33	Makamusi.....	41
3.4	Shule, Taasisi na Vyu.....	43
3.5	Semina za ukuzaji wa Kiswahili.....	47
3.6	Kasoro za juhudi hizi za ukuzaji wa Kiswahili.....	50
3.7	Hitimisho.....	57
3.8	Tanbihi.....	58

SURA YA NNE

4.0	Maoni na mapendekezo kuhusu ukuzaji na uendelezaji mwema wa Kiswahili.....	60
4.1	Utangulizi.....	60
4.2	Ukuzaji wa Kiswahili kulingana na Ulimwengu wa sasa.....	61
4.3	Yanayopaswa kufanywa ili Kiswahili kikuzwe kote kama lugha moja.....	66

4.4	Umuhimu wa kukikuza Kiswahili.....	71
4.5	Hitimisho.....	74
4.6	Tanbihi.....	78
	<u>MAREJEO</u>	80

SHUKRANI

Watu wengi wamenisaidia katika kazi hii. Kwa wote natoa shukrani zangu za dhati. Hasa shukrani zangu ziwaendee Profesa Karega Mutahi na Dakta Jay Kitsao kwa usimamizi wao mwema ambao umeitoa kazi hii katika lindi na kuifanya ifaayo kusomwa. Mchango wao ulikuwa mkubwa.

Wahadhiri wengine wa Idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika hususa Mwalimu Kazungu Kadenge na Kithaka wa Mberia wamenifaa kwa mchango wao wenye maadili bora katika nyanja hii na kwa hivyo sina budi kuwashukuru.

Wanafunzi wenzangu ambao waliniauni siku hata siku, hasa Habwe, J.H. na Mbatia, A.M. nawashukuru.

Namshukuru pia mamangu mpenzi Joinah Mukhwana kwa kuniruhusu kufanya kazi yangu kila nilipomtaka radhi ya kutokwenda kondeni wakati wa likizo.

Mwisho, shukrani zangu ni kwa mpigaji taipu Bi. L. Mungai ambaye bila kuishughulikia kazi hii vilivyo ingekuwa na kilema.

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI WA UTAFITI

Madhumuni yetu katika kazi hii ni kujadili ukuzaji wa Kiswahili kwa kuangalia jitihada ambazo zimefanywa pamoja na zile ambazo zinafanywa kukipanua Kiswahili kulingana na mahitaji ya kisasa. Tutaanza utangulizi wa kazi hii kwa kuangalia sababu za kuchagua somo hili, kisha twende kwenye lengo la tasnifu, tatizo linalofanyiwa utafiti huu, yaliyoandikwa kuhusu somo hili na njia za utafiti. Tutaeleza kwa tafsili kila mojawapo ya vipengee hivi ili vitufae katika kuishughulikia kazi hii.

1.1 SABABU ZA KUCHAGUA SOMO HILI

Kutokea tarehe 26.10.1987 hadi tarehe 29.10.1987 kulikuwa na semina ya kushughulikia Kiswahili mjini Dar es Salaam. Semina hii ilivutia wadhamini wa kima-taifa ukiwemo ubalozi wa Ujapani, Jamhuri ya Ujerumani Magharibi, Uchina na Sweden.¹ Isitoshe, UNESCO ina historia ndefu ya kudhamini semina kama hizi. Hali hii, ya kudhamini semina zilizolengwa katika kukikuza kiswahili, ndiyo iliyotutia hamasa ya kulichagua somo hili ili kudadisi kiswahili kikuzwe vipi kusudi kiweze kujitosheleza katika shughuli zake za mawasiliano.

Kiswahili ni lugha ya saba katika lugha za ulimwengu.² Kwa sababu hii chahitaji kukuzwa ili kibakie katika wadhifa huu. Pia, Kiswahili chahitaji kukuzwa ili labda siku moja ije izipite baadhi ya lugha nyingine

kuu kwa umaarufu hasa tukizingatia kuwa ndiyo lugha ya pekee kutoka barani Afrika iliyoenea kwingi. Lakini ili kukikuza vema Kiswahili hatuna budi kurejelea historia yake hata ikiwa ni kwa muhtasari tu. Hivyo basi sababu mojawapo ya kuchagua mada hii ni kuangalia kukuzwa kwa kiswahili katika misingi yake ya kihistoria.

1.2 LENGO LA TASNIFU

Hali na hadhi ya Kiswahili katika nchi zote tatu za Afrika Mashariki yatofautiana. Sababu kubwa inayotolewa na Whiteley (1969) ni kwamba kila mojawapo ya nchi hizi ilirithi sera tofauti ya lugha kutoka kwa wakoloni wa kizungu. Katika kuangalia mada yetu ya utafiti tutakuwa na lengo la ama kukanusha au kukubaliana na rai hii kwa kudadisi jinsi Kiswahili kilivyokuzwa katika enzi za wakoloni hawa. Yaani tutajaribu kuona ikiwa kila nchi ya Afrika Mashariki ilikuwa ikijikuzia kiswahili kivyake - hali ambayo ilisababisha kuweko kwa tofauti za hali na hadhi ya lugha hii baada ya uhuru.

Kiswahili kimesambaa na kinatumika kwingi katika Afrika Mashariki na Kati. Lengo letu jingine ni kuonyesha jinsi ambavyo Kiswahili, kwa maoni yetu, chaweza kukuzwa kama lugha ya kisasa ili kiweze kukidhi mahitaji ya kimawasiliano katika nyanja mbali-mbali za kijamii bila kukwama au kuzusha maswali

juu ya dhana au istilahi fulani.

Kiswahili kilidharauliwa na baadhi ya watu wakati wa enzi ya ukoloni wa Mzungu (Tazama Lema, A Mulika Na. 2 uk. 3). Hata hivyo, baada ya nchi za Afrika Mashariki kujipatia uhuru viongozi wake waliiona lugha hii kama kiunganishi cha watu wa matabaka na makabila mbalimbali. Kwa sababu hii, viongozi hawa walihimiza matumizi ya lugha hii. Katika nchi ya Tanganyika (kwa sasa Tanzania Bara) Kiswahili kilifanywa lugha ya taifa punde tu baada ya nchi hiyo kujipatia uhuru. Katika tasnifu hii mojawapo ya malengo yetu ni kujadili juhudi zilizofanywa na Afrika Mashariki na hata ulimwengu wote kwa jumla katika kukikuza na kukiimarisha kiswahili baada ya kukigundua kuwa silaha muhimu ya umoja.

1.3 UPEO NA MIPAKA YA TASNIFU

Mada yetu ya utafiti ni pana na inaweza kuhitimishwa kwa jinsi nyingi kutegemea mitazamo na misimamo ya wachunguzi mbalimbali. Kwa upande wetu, tutauchukua mwaka 1930 kama mwanzo wa kazi yetu ya utafiti. Hitimisho litakuwa ni wakati wa sasa. Ingawa tumeweka mipaka hii, inapotulazimu hatutakuwa na budi kuikiuka ili tupate mwendelezo mwema wa hoja.

Tasnifu hii itagawanyika katika sehemu nne. Sehemu ya kwanza ni utangulizi wa kazi yenyewe. Sehemu ya

pili itazingatia usanifishaji wa Kiswahili kuanzia mnamo mwaka 1930 na athari zake kwa lugha hii. Sehemu ya tatu itazungumzia njia ambazo zimetumiwa katika kukikuza Kiswahili Afrika Mashariki na kati hasa baada ya Uhuru.

Halafu sehemu ya nne, ambayo itakuwa ni hitimisho la kazi yetu ya utafiti, itatoa mapendekezo kuhusu jinsi kiswahili kinavyostahili kukuzwa ili kufahamika kote na kukabiliama kikamilifu na hali yasasa ya kisayansi na kiteknolojia. Pia sura hii itazungumzilia, japo kijuujuu tu, umuhimu wa kukikuza kiswahili.

1.4 TATIZO LINALOTAFITIWA

Tunatafiti juu ya ukuzaji wa Kiswahili. Kwa hivyo tutaangalia juhudi ambazo zimefanywa katika kuikuza lugha hii ili kupanua mawasiliano baina ya watumiaji wake. Maswali ambayo yanatafitiwa majibu ni: Je, kwa nini Kiswahili kikuzwe? Je, lugha ya Kiswahili imekuwa ikikuzwaje? Katika kukuzwa hivyo, kumekuwa na upungufu gani? Na je, ni mapendekezo gani ambayo yangeweza kutolewa ili yakifuatwa lugha hii iwe yakuzwa ipasavyo?

1.5 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI

Ukuzaji wa Kiswahili ni mada ambayo imevutia wasomi wengi kama nyanja muhimu ya utafiti.

Maganga, C. (1983) ameandika makala kuhusu somo hili na kuyaita Juhudi za ukuzaji wa Kiswahili Tanzania bara. Mwaka huo huo (1983) Akida, H. pia ameandika makala kuhusu somo hili na kuyaita Ukuzaji na undelezaji wa msamiati wa Kiswahili, naye Gibbe, A.G. (1983) ameandika kuhusu Maendeleo ya istilahi za Kiswahili.

Baadhi ya waandishi wengine ambao wamezungumzia, kugusia au kutaja ukuzaji wa Kiswahili in Whiteley, W (1969), Chiraghdin, S na Mnyampala, M.E. (1977), Mbaabu, I (1978), Mbeo, F.E. (1971), Kiingi, B.K. (1984) na Nkwera, F.V.M. (1978).

Ijapokuwa mada hii imeshughulikiwa na wengi, kwa maoni yetu, baadhi ya yaliyoandikwa hayaridhishi kwa jinsi ambavyo wengi wao wamelileta somo la ukuzaji wa Kiswahili kama mada-tegemezi tu na kwa hivyo wakakosa kulipa uzingativu wa kutosha. Isitoshe, wengi wao wamelitazama somo hili katika misingi na mazingira ya kikwao tu kama kwamba Kiswahili si kimoja kote. Fauka ya haya, walikuwa na mipaka ambayo ni tofauti na yetu. Kwa sababu hii, ni matumaini yetu kuwa kazi hii itazama kuliko zile nyingine.

1.6 NJIA ZA UTAFITI

Mradi suala la ukuzaji wa Kiswahili limeshughulikiwa

na wengi, shughuli zetu nyingi kuhusu utafiti wa somo hili zitakuwa katika maktaba ambapo vitabu na majarida mbalimbali yanayolizungumzia suala hili yatarejelewa. Katika kufanya hivi, tutakusanya takwimu zifaazo kwa kazi yetu ya utafiti na hivyo zitatuchangizia katika utafiti.

Njia ya pili tutakayoitumia katika utafiti wetu ni ile ya kuhoji wataalamu wa Kiswahili katika nyanja ya historia na maendeleo yake. Hivi, tutajadiliana na kushauriana nao kiasi kwamba yale masuala ambayo kwetu huenda yakaonekana kuwa magumu yatajadiliwa na kurahisishwa kwa manufaa ya wapenzi na watumizi wa lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, kabla ya kukubali maoni na michango ya wataalamu hawa tutachanganua yote watakayosema na kuyatia mahali pafaapo.

Njia nyingine itakayotumiwa katika utafiti wetu ni ile inayohusu tajriba zetu. Hapa tutatumia ujuzi wetu ama tuliofunzwa au tuliojifunza wenyewe kuhusu Kiswahili na maendeleo yake.

Halafu njia ya nne tutakayoitumia inahusu kusikiliza vipindi mbalimbali redioni na kutazama televisheni. Vipindi vifuatavyo na ambavyo hulijadili suala hili la ukuzaji wa Kiswahili vitatufaa katika kazi hii: Lugha Yetu na Ukumbi wa Kiswahili vya Idhaa ya Kiswahili ya Sauti ya Kenya, na Mbinu za Kiswahili

cha Idhaa ya Kiswahili Redio Tanzania, Dar es Salaam.

Hizi njia nne ndizo tatakazozitumia katika utafiti wetu. Hata hivyo, endapo njia nyingine, ambayo hatukuitaja, itajitokeza na tuone kuwa inaweza kutufaa, hatutakuwa na budi kuitumia.

1.7 HITIMISHO LA MWONGOZO

Mwongozo huu unalenga katika kuifanya kazi yetu ya utafiti kuwa rahisi. Twadhani kuwa mwongozo huu umetumulikia hatua zetu zote katika kazi hii na kuifanya kuwa timilifu.

1.8 TANBIHI

1. Tazama gazeti la Daily News la Tanzania
la tarehe 21.10.87 uk. 3 chini ya kichwa:
Kiswahili Seminar Open in Dar es Salaam on Monday

2. Chiraghdin, S. na Mnyampala, M.E. katika
Historia ya Kiswahili, O.U.P., Nairobi (1977)
uk. 67.

SURA YA PILI

2.0 USANIFISHAJI WA KISWAHILI (1930)

2.1 UTANGULIZI

Lugha huwezesha wanadamu kuwasiliana na kila mtumiaji wa lugha huitumia kibusara ili maana aliyoik-usudia ipate kujitokeza waziwazi. Lakini isichukuliwe kuwa mradi lugha yatumika kwa mawasiliano basi kila mtumiaji ana uhuru wa kwenda kokote hata, kwa mfano, akajiundia maneno na kuanza kuyatumia papo kwa papo. Hili likifanywa mawasiliano yatakwama kwa kuwa huenda pakatokea hali ya kutokukubaliana kuhusu miundo ya baadhi ya maneno na pia maana zake. Ni kwa sababu hii ndipo hali ya kusanifishia lugha hujitokeza kama jambo muhimu na la lazima.

Usanifishaji wa lugha ni utaratibu ambao unawezesha lahaja moja ya lugha fulani kukubaliwa kote katika eneo la wazungumzaji wa lugha hiyo kama lahaja 'bora' na yenye hadhi. Ingawa lahaja moja huchaguliwa kama iliyo 'bora' kutoka miongoni mwa lahaja nyingine zote, hii haimaanishi kuwa lahaja hizo nyingine zilizoachwa hazifai kwingineko. Aghalabu utaratibu wa kusanifisha lugha hushugh^ulikiwa na wanaisimu wakizingatia mambo mbalimbali ambayo si sana kujulikana watu ambao si wanaisimu. Lakini kwa jumla dhana ya usanifishaji wa lugha inahusu haja za kuongeza makubaliano baina ya watumiaji wa lugha fulani. Kutokana na kusanifishwa

kwa lugha basi, sheria za kutamka maneno na za sarufi huundwa, namna ya kuandikwa kwa lugha hiyo pia hushughu-likiwa, msamiati wa lugha hiyo hupanuliwa n.k.

Kuna sababu nyingi za kuchaguliwa lahaja moja ² ya lugha kuwa kielelezo cha lugha hiyo na kuitwa lahaja sanifu. Ingawa sababu hizi huhitilafiana kutoka nchi moja hadi nyingine, kinachoonekana ni kuwa lugha sanifu ni lahaja ambayo, kwa sababu za kihistoria na za kiisimu ambazo ni za 'kiajali', hufanywa kuwa muhimu¹ miongoni mwa lahaja nyingine. Kwa ufupi, sura hii inadhamiriwa kuangalia sababu zilizokifanya Kiunguja kichaguliwe miongoni mwa lahaja zote za Kiswahili kama lahaja ambayo ingekuwa msingi wa Kiswahili sanifu. Pia, sura hii inadhamiria kujadili kasoro zisemwazo kuwa zinajitokeza na kusanifishwa huku kwa kiswahili, na ni kwa vipi usanifishaji wa kiswahili umekifanya kuwa kimoja kote kizungumzwako.

2.2 MASIALA YALIYOSABABISHA USANIFISHAJI WA KISWAHILI

Kabla ya kusanifishwa kwa Kiswahili kulikuwa na harakati mbalimbali za matumizi ya lugha hii ambazo tunaweza kusema kuwa ndizo zilizosababisha haja ya kusanifishwa kwa Kiswahili. Kukua na kuenea kwa majimbo ya mwambao wa Afrika Mashariki kiuchumi na kisiasa kulianzisha hatua za mwanzo za kueneza lugha ya Kiswahili na uanzishaji wa enzi ya Wamanga² Zanzibar mwakani

1840 ilikuwa ni hatua ya pili iliyosaidia kukieneza Kiswahili katika bara ya Afrika.³ Halafu yakaja Mapinduzi ya Viwandani. Kutokana na uanzishaji wa viwanda, bidhaa nyingi zilizotengenezwa zilikosa soko. Isitoshe, kadiri muda ulivyo zidi, malighafi kwa viwanda hivi yalianza kuadimika; ikawa lazima masoko na mahali pa kupata malighafi patafutwe. Afrika Mashariki ilijitokeza kuwa mojawapo ya mahali ambapo soko kwa bidhaa za viwandani na pia ambapo malighafi ya viwanda yangepatikana. Basi watu walitoka Ulaya, Marekani, Bara Hindi n.k. na kuja janibu hizi wakiwa na malengo yaliyotajwa hapo juu. Baada ya kuja huku walijifunza Kiswahili katika pwani kabla ya kuingia bara maana wakati huo lugha hii ilikuwa kama 'ufunguo'⁴ wa kuingilia bara.

Watu hawa wakiwa bara hawakuwa wakitumia Kiswahili cha aina moja kwa kuwa lahaja za Kiswahili ni nyingi na

Waswahili wamesambaa katika Bara la Afrika kwa urefu wa kilomita 1500 kuanzia Mto Liro, ... mpaka mlango wa Mto Juba, na vile vile sehemu za Banadiri (Marka, Barawa) na Visiwa vya Magunyani na Amu, Wasini na Funzi, ..., na Masiwani ... hata sehemu za Bukini (Madagascar), na kwa upana wa baina ya kilomita tano na kumi.⁵

Ikiwa basi kuna lahaja nyingi za Kiswahili na lahaja hizi zimetengwa na sura mbalimbali za kijiografia, ni dhahiri kwamba wageni waliokuja Afrika Mashariki

hawakutumia Kiswahili aina moja - hali ambayo, haikosi, ilizusha mvutano baina ya wageni hawa. Hili linajitokeza wazi Edward Steere na Ludwig Krapf wanapozozana kuhusu Kiswahili bora kati ya Kimvita na Kiunguja kiasi cha Krapf kuweza kukiita Kiunguja Kiswahili kijingajinga'.

Kwa ufupi tunasema kwamba lugha ya Kiswahili ilizidi kukua kwa kupata wazungumzaji zaidi kadiri Afrika Mashariki ilivyokumbana na matukio mbalimbali ya kihistoria. Lakini hali ya mvutano iliyokuweco baina ya wazungumzaji wa lahaja mbalimbali ilijitokeza na haja ya kusanifisha Kiswahili ili kionekane kuwa ni lugha moja.

Kabla ya kukisanifisha Kiswahili kulikuwa na fikra kuhusu kupatikana kwa lugha moja ambayo ingeweza kutumika katika eneo zima la Afrika Mashariki, hasa katika uwanja wa elimu. Mwaka 1920 wamisheni, ambao wakati huo walisimamia shughuli nyingi za kielimu, waliamua kukitumia Kiswahili Kiunguja kwa kuhubiria na kufasiria dini kote Tanganyika. Mwaka 1924 Serikali ya Kiingereza Tanganyika iliamua Kiunguja kiwe ndiyo lugha ya kutumiwa na watu wote katika mafunzo. Wakati huo pia Serikali hiyo ilipendekeza Kiunguja kifanywe Kiswahili Sanifu ili kiwe ni lugha ambayo ingekuwa kipimio cha usahihi miongoni mwa lahaja nyingine

zote za Kiswahili. Basi juhudi za kutaka kuisanifisha lugha ya Kiswahili zilikuwa zimeanza nazo zikilenga katika kukichagua Kiunguja kama lahaja sanifu.

Katika historia ya usanifishaji wa Kiswahili, tume ya Phelps-Stokes ~~Commission~~ haiwezi kusahaulika. Kikundi hiki cha wasomi kilikuwa na watu ambao, wengi wao walitoka Marekani (U.S.A.) na baada ya kuja Afrika Mashariki na kuitalii hali ya elimu (hasa Tanganyika) kwa upande wa Waafrika, walitoa mapendekezo kadhaa ambayo yaliwapa wakoloni mtazamo mpya kuhusiana na elimu ya Waafrika. Baada ya tume hii kuchapisha ripoti yake - ripoti iliyowasisimua wanaelimu - wakoloni waliitisha kongamano Dar es Salaam mwaka 1925.

Mkutano huu uliosimamiwa na Gavana wa Tanganyika ulijadili suala la lugha miongoni mwa masuala mengine. Kuhusu lugha, mkutano huu ulijadili lugha ambayo ingefaa kufunziwa shuleni ili kuwe na mfumo wa elimu ulio sare kote nchini. Kiswahili kwa kuwa ndiyo lugha iliyokuwa ikieleweka kote nchini Tanganyika ilichaguliwa kwa madhumuni hayo maana kilionekana ni lugha ambayo ingetosheleza mahitaji ya shughuli za elimu na zile za serikali kwa vile kilivyokuwa kinafahamika katika sehemu kubwa ya Afrika Mashariki na ya Kati⁶. Katika mkutano huo wa Elimu wa 1925, ilichaguliwa kamati ambayo jukumu lake lingekuwa ni kushughulikia uwezekano wa kupata lahaja moja miongoni

mwa lahaja za Kiswahili ili lahaja hiyo itumike katika shughuli za mawasiliano rasmi nchini Tanganyika.

Kufuatia mkutano wa 1925, mnamo mwaka 1926 mapendekezo fulani yalitolewa kuhusu kutamkwa na kuandikwa kwa maneno ya Kiswahili. Yaani, suala kuu katika mapendekezo hayo lilikuwa ni, je, mpaka kati ya maneno uwe wapi? Pamoja na mapendekezo, vilipendekezwa pia vitabu ambavyo vilihitajika vizingatie mapendekezo hayo. Kutokana na juhudi hizi za mwaka 1926, mwaka huo huo majaribio yalifanywa katika gazeti la MAMBOLEO na yalihusu matumizi ya 'C' badala ya 'C', na 'Ŋ' badala ya 'ng'. Haya mapendekezo yalikataliwa na Idara za Elimu nchini Tanganyika (Whitely 1969).

Nchini Kenya pia kulikuwa na fikira kuhusu kupatikana kwa lugha moja ambayo ingetumiwa katika shughuli za elimu shuleni. Mwakani 1927 Serikali ya Kenya iliitisha mkutano ambao madhumuni yake yalikuwa ni kujadili umoja wa Kanuni za Lugha ya kutumiwa shuleni.⁷ Baada ya kugundua kwamba Kenya pia ilikuwa na tatizo la lugha, Tanganyika ikataka ushirikiano katika kulitfutia tatuzi suala hili. Kufuatia rai hii ya Tanganyika mwakani 1928 nchi zote nne za Afrika Mashariki - Kenya, Uganda, Tanganyika na Zanzibar - zikawatuma wajumbe Mombasa ambako kulikuwa na mkutano uliojadili suala la ni lahaja gani ya Kiswahili iliyopasa kutumika

kama msingi wa usanifishaji wa Kiswahili.

Wajumbe wa mkutano huo wa Mombasa waliomba kibali cha kuunda kamati ambacho walipewa. Baada ya kamati hii ya mwakani 1928 kuundwa ilikabiliwa na tatizo la lahaja ambayo ingechaguliwa kuwa ni kielelezo cha Kiswahili sanifu. Nafasi ya lahaja hii iling'ang'aniwa na lahaja tatu muhimu za Kiswahili ambazo zilikuwa Kiamu, Kimvita na Kiunguja. Baada ya muda fulani, Kiamu kilishindwa nguvu na zikabaki lahaja za Kimvita na Kiunguja zikimenyana mpaka baadaye kiunguja kika-jitokeza kama mshindi, hasa kwa sababu kilikuwa kimeenea katika eneo kubwa zaidi la Afrika Mashariki ikilinganishwa na lahaja zile nyingine.

Kufuatia kukubaliwa kuwa kiunguja kitumiwe kama msingi wa kusanifishia kiswahili, mwakani 1929 Katibu wa Halmashauri ya Magavana wa Afrika Mashariki aliziandika serikali hizo nne kuhusu suala la kubuniwa kamati ya lugha ya serikali zote nne. Serikali hizo zote zilikubali na zikataka idhini ya kufanya hivyo kutoka kwa Waziri wa Makoloni. Aliwakubalia na tarehe 1.1.1930 Kamati ya Kiswahili iliyoitwa Inter Territorial Language (Swahili) Committee ilibuniwa ili kukisanifisha Kiswahili.

2.3 USANIFISHAJI WA KISWAHILI NA KASORO* ZAKE

Kwa maoni ya baadhi ya wachunguzi wa historia

* Hatukubaliani na Kasoro hizi kidhati.

na maendeleo ya Kiswahili, katika kusanifisha lugha hii kulitokea dosari moja kuu: nayo ni kuchaguliwa kwa Kiunguja kama msingi wa lugha sanifu. Kosa hasa ni kwamba wataalamu waliokuwepo ama hawakufahamu au walijitia kutokujua kuhusu lahaja ya Kiswahili yenye kina na ndiyo sababu wakakichagua Kiunguja. Lau wangefahamu lahaja ya Kiswahili yenye kina wange-kichagua Kiamu. Hii ni kwa sababu Lamu ndiko maandishi ya Kiswahili katika hati ya Kiarabu yalipochipukia. Isitoshe, ndiko ushairi wa Kiswahili ulikuwa umeendelea kwa muda mrefu. Fauka ya haya, Lamu ni sehemu iliyo katika eneo ambamo Kiswahili kilichipukia. Zote hizi ni shughuli zilizochangia lugha ya Kiswahili na kuipanua. Waambavyo wana-historia-mapokeo kuwa asili ya Kiswahili ni kaskazini⁸, hatuoni ni kwa nini lahaja hii ya kaskazini iliyo katika eneo lilo hilo kilipochimbukia Kiswahili na kuenea kwingineko haikuweza kuchukuliwa kama msingi wa kukisanifisha Kiswahili. Hata hivyo, kuna sababu moja kuu ya kutochaguliwa kwa Kiamu nayo ni kwamba lahaja hii haikuwa na wazungumzaji miongoni mwa wamisheni. Kimvita pia hakingeweza kuchaguliwa maana watetezi wa Kiunguja walikuwa wengi kuliko wale wa Kimvita. Kwa kuwa na idadi kubwa ya Watetezi hili ni dhahirisho kuwa lahaja ya Kiunguja ilikuwa maarufu miongoni mwa lahaja nyingine za Kiswahili. Kwa hivyo basi ni makosa

kusema kuwa kuchaguliwa kwa kiunguja kuwa msingi wa kukisanifisha Kiswahili kuna kasoro maana kama tulivyo-kwishitaja katika utanglizi wa sura hii lugha sanifu ni lahaja ambayo, kwa sababu za kihistoria na za kiisimu ambazo ni za kiajali hufanywa kuwa muhimu miongoni mwa lahaja nyingine. Basi kama historia ya Kiunguja wakati huo pamoja na isimu ya lahaja hii vilikifanya Kiunguja kionekana bora miongoni mwa zile lahaja nyingine kuchaguliwa kwake hakuna kasoro.

~~T~~unachosema hapa ni kwamba hata kama kuchaguliwa kwa Kiunguja ni kasoro, Kasoro hii haikuwa ya kujitakia kwa upande wa waliokichagua. Wakati huo mji wa Unguja ilikuwa ndio Makao Makuu ya wageni waliokuja Afrika Mashariki. Basi wageni wengi waliokuja janibu hizi wakawa wanajifunza Kiunguja mwanzo. Isitoshe, vitabu vingi vya Kiswahili vilivyoandikwa kwa hati ya Kilatini vikawa vyatoka Unguja. Basi kulipotokea pendekezo kuwa lahaja moja ichaguliwe na kupewa hadhi, wataalamu wengi wakapendekeza Kiunguja kitumiwe kama msingi wa kuundia Kiswahili sanifu.

Kuna rai kwamba Kiswahili Sanifu Katika kuundwa kulikuwa na madhumuni ya kuirahisisha kazi ya utawala kuliko kuleta manufaa kwa wenyeji wa nchi hizi maana Waafrika walianza kuchaguliwa kuwa washiriki wa kamati

ya kusanifisha Kiswahili mwakani 1939 na hawakushiriki katika mashauri ya kamati hii mpaka mwaka wa 1946 (Chiraghdin, S 1977: 58-9). Ni vigumu sana kuyatambua kwa hakika 'manufaa' yanayozungumziwa hapa. Kwa maoni yetu, manufaa haya ni kule kushirikishwa kwa Waswahili 'wenyewe' Katika shughuli hii ya usanifishaji wa Kiswahili. Hakika ingefaa zaidi kama Waswahili 'wenyewe' wangeshirikishwa ili kutoa maoni kuhusu miundo ya baadhi ya maneno yalio-ingizwa katika Kiswahili kusudi kukipanua. Hata hivyo, jambo moja lifahamike. Hütuna ushahidi kuhusu Waswahili ambao walikuwa wamehitimu katika isimu ya lugha. Basi tunaweza kusema kuwa ukosefu wa wanaisimu miongoni mwa Waswahili ndiyo sababu kuu ya kutowashirikisha katika shughuli za mwanzo za kukisanifisha kiswahili maana mtu asiyeijua isimu ana hatari ya kuivuruga lugha kwa kuelekeza kokote kwa kuwa huwa hana misingi madhubuti ya kazi hiyo. Hapa tuna maana kwamba kujua lugha kwa kuzaliwa katika jamii fulani ni tofauti na kuisomea lugha. Hii ndiyo maana Wazungu, akiwemo Profesa Carl Meinhof mwenye ujuzi wa lugha za Kibantu, wakawa ndio wa kukikuza na kukiendeleza Kiswahili katika misingi ya historia ya ukuzaji wa lugha. Ni kwa sababu hii ndiyo ilisemwa na wataalamu hawa kuwa juhudi zingefanywa kukuza Kiswahili kwa kukiielekeza kwenye Ubantu lakini pale ambapo maneno ya Kiarabu au ya lugha nyingine

yatumika na yameshika pangeachwa hivyo.⁹

Kufungamana na kukuzwa kwa Kiswahili kwa kuelekeza kwenye Ubuntu kuna baadhi ya wachunguzi (akiwemo Nkwera, FVM: 1978) ambao wamefasiri kifungu hiki kuwa na maana kwamba ni Kiunguja tu kilichotumiwa huku lahaja nyingine zikiwa zadharauliwa. Hivi sivyo uhalisi wa mambo ulivyo maana Kiswahili ni Kibantu na kwa hivyo inaposemwa kielekezwe kwenye Ubuntu ina maana kuwa lahaja za Kiswahili ambacho ni Kibantu pia zingeangaliwa pamoja na lugha nyingine za Kibantu. Kwa maoni ya wachunguzi kama hawa basi, kujifunga kwa kiunguja kwa kukikuza Kiswahili sanifu ni kosa ambalo lilifanywa na kamati ya usanifishaji wa lugha hii. Kwetu hili si kosa maana fasiri yao na yetu haziingiliani.

* Istoshe, ifahamike kuwa lahaja fulani inapofanywa msingi wa usanifishaji haimaanishi kuwa iko pale kwa jina tu bali huwa imepewa ule wadhifa wa utukufu na ubora na kwa hivyo haiwezi kulinganishwa au kupimwa katika mizani moja na lahaja nyingine za lugha hiyo.

Fauka ya haya, kama anavyosema Langacker, R.W. (1968:55) Kila lahaja ya lugha ina uwezo wa kujitosheleza na pale ambapo haijitoshelezi ina uhuru wa kufanya chochote kile ili ijitosheleze. Kwa sababu hii, hapana mantiki katika kusema kuwa Kiswahili sanifu kina upungufu kwa sababu ya kuichagua lahaja ya Kiunguja tu kushughulikiwa na kuendelezwa na kuziona lafudhi nyingine za Kiswahili

kuwa ni lahaja zisizokuwa na umuhimu mkubwa.¹⁰

Katika kukichagua Kiunguja na 'kuzipuza' lahaja nyingine kamati ya kusanifisha Kiswahili ilitambua kwamba bila kufanya hivyo haingepiga hatua yoyote kwa kuwa pangukuwa na mvutano baina ya lahaja, kila moja iking'ang'ania nafasi iliyo kubwa. Ni maoni yetu pia kuwa ni kwa kuhofia vurugu ambalo lingetokea kila Mswahili akitetea lahaja yake ndiy^o kamati ya usanifishaji wa Kiswahili ikakosa kuwashirikisha Waswahili 'wenyewe' mpaka kuanzia miaka ya arobaini.

Chiraghdin, S. na Mnyampala, M.E. (1977:60) wasema kuwa kasoro nyingine ya Kiswahili Sanifu ni kuwa shuleni wanafunzi wa Kiswahili walikuwa wakifunzwa Kiswahili na wageni (Wazungu na wenyeji) waliofunzwa 'Kistandard' na Wazungu hao. Eti wanafunzi hawa Waswahili walikuwa wakiambiwa kuwa lugha yao wenyewe kama walivyokuwa wakiitumia ilikuwa siyo. Eti walilazimishwa kufuata mpango na sarufi na matumizi ambayo 'mafundi wa Kiswahili' walitaka. Kwa maoni yetu kufunzwa Kiswahili hivi hakuna kasoro yoyote. Lugha Sanifu huwa hivyo popote na kwa hivyo katika kuwafunza wanafunzi wa Kiswahili lugha yao jinsi ilivyofanywa wasanifishaji walikuwa na lengo la kuiimarisha lahaja ya Kiunguja kama msingi wa Kiswahili Sanifu. Basi hatuwezi kuwalaumu walimu waliowakosoa wanafunzi mathalani wa Kimvita

wakisema 'mtomo' badala ya 'mchomo' kwa kuwa katika Kiswahili Sanifu kila mojawapo ya maneno haya lilikuwa limewekwa mahali pake.

Yaonekana wazi kuwa kuchaguliwa kwa Kiunguja kuwa msingi wa usanifishaji wa Kiswahili kulitokea kwa sababu ya wakati na pia hali ya lugha hii. Lahaja ya Kiunguja ilikuwa ikitumika kwingi katika shughuli za kila siku na kwa hivyo kuwarudisha watu wengi nyuma kwa kuwaambia kuwa Kiswahili chao hakitakiwi ingekuwa vigumu sana kukubalika. Hata tukikubali kuwa Kiswahili Sanifu kina kasoro zinazotokana na juhudi za wasanifishaji wa lugha hii, sharti tukumbuke kuwa kasoro hizi hazikuwa za kujitakia. Isitoshe, baadhi ya kasoro hizi zafikirika tu katika akili za baadhi ya wachunguzi wa suala hili wakiwemo akina Nkwera, F.V.M. na Chiraghdin, S. Kama tulivyokwisha gusia. Wachunguzi hawa hawalijadili suala hili kwa kuchunguza pande zote mbili ili kueleza manufaa na kasoro za usanifishaji wa Kiswahili, na ikiwa kuna kasoro hawajiulizi kwa nini kasoro hizi zikatokea. Hapa kinachojidhihirisha ni kwamba wazitajao kasoro hizi mara nyingi huwa hawazirejelei historia za lugha nyingine pamoja na uhalisi wa mambo katika misingi ya historia ya lugha ya Kiswahili wakati huo.

2.4 MANUFAA YA USANIFISHAJI WA KISWAHILI

Manufaa ya kwanza yaliyotokana na usanifishaji

wa Kiswahili yanahusu kukuzwa na kusambazwa kwa lugha hii, hali ambayo imeitafutia nafasi na hadhi miongoni mwa lugha kuu za ulimwengu. Yaani kutokana na kusanifishwa kwa Kiswahili, juhudi za pamoja zilianza kufanywa ili kukikuzwa kama lugha moja; na hivi sasa lugha hii yatumika kwingi kiasi cha kuipa nafasi ya saba ulimwenguni kote.

Kutokana na juhudi za kuisanifisha na kuikuzwa lugha ya Kiswahili mawasiliano yalisahilishwa kote katika Afrika ya Mashariki na ya Kati.

Usanifishaji huu wa Kiswahili ulileta mwingiliano wa moja kwa moja kilugha kati ya watumiaji wa Kiswahili kinyume na hapo awali ambapo kila watu walikuwa wakijizungumzia Kiswahili chao kivyao.

Kamati ya usanifishaji wa Kiswahili ilipendekeza vitabu ambavyo iliviona kuwa mwafaka katika matumizi ya shuleni. Vitabu hivi vyote vilikuwa vimeandikwa katika Kiswahili Sanifu. Kama tujuavyo, vitabu ni zana muhimu sana katika ukuzaji na usambazaji pamoja na uimarishaji wa lugha. Kwa kutambua hili wasanifishaji wa Kiswahili waliwatia moyo waandishi wa vitabu kwa kuwapa tunu. Katika uwanja huu huu wa usanifishaji na ukuzaji wa Kiswahili kimaandishi makamusi yakiwa ni kifaa muhimu katika kuikuzana kuisambaza lugha, hayakupuuzwa. Kwa mfano, kamusi ya Madan iliyoitwa

Swahili-English na English-Swahili ilianza kushughulikiwa tena upya huku vitomeo vilivyokuwemo vikirekebisha ili vizingatie mfumo ambao ulitakikana na Kiswahili Sanifu. Hizi zote zilikuwa ni juhudi zakukikua Kiswahili kimaandishi na si ajabu waandishi kadhaa walijitokeza na kuandika vitabu vya Kiswahili ambavyo baadhi vingali vikitumiwa hata sasa. Baadhi ya watu walioandika vitabu ni Shabaan Robert aliyandika Adili na Nduguze (1952); C.A. Sharif Omar aliyandika Hadithi za Hazina Binti Sultan (1951) na H.L. Riwa aliyandika Hadithi za Rafiki Saba (1951). Kwa kuwa vitabu hivi viliandikwa kwa Kiswahili Sanifu, vilisaidia sana katika kuikuza lugha hii katika mwelekeo huu mpya.

Wakati juhudi hizi zilipokuwa zikifanywa ili kuwachochea hima waandishi wa vitabu vya Kiswahili, tafsiri mbalimbali zilikuwa zikiingizwa katika Kiswahili. Hali hii ilitokana na kuhitajika kwa vitabu vya Fasihi ya Kiswahili^{ll} ambavyo wakati huo vilikuwa vichache sana. Ni kwa sababu hii ndiyo tafsiri kama Mashimo ya Mfalme Suleiman, Alfu Lela Ulela, Hekaya za Abunuwasi n.k. zikaingizwa katika uwanja wa Fasihi ya Kiswahili. Licha ya tafsiri hizi kuwaelekeza waandishi wa Kiafrika kama vile Shabaan Robert, ziliwasaidia pia wale waliokijua Kiswahili pekee kupata mawazo yaliyokuwa katika vitabu hivi lakini ambayo wasingepata lau vitabu hivi visingetafsiriwa.

Kuhusu tafsiri hizi kukichafua Kiswahili kimuundo kama wanavyodai akina Chiraghdin, S na Mnyampala, M.E. (1977), ni muhimu kukumbuka kuwa siyo tafsiri zote ambazo huchafua lugha, tukizingatia kuwa kuna nadharia za tafsiri ambazo hufuatwa katika kuifanya kazi hii. Maoni yetu kuhusu suala hili ni kwamba tafsiri hizi hazikuchafua muundo wa Kiswahili bali ziliikuza lugha hii kimuundo. Hii ni kwa sababu Kiswahili Sanifu ni lugha yenye maneno mengi sana na kanuni za sarufi yake zinaruhusu mnyumbuko mkubwa unaotuwezesha kabuni maneno ya miundo ya kila namna na kuyazungumza kwa ufasaha usio na mfano katika lugha nyingine¹². Hapa tuna maana kuwa kuja kwa tafsiri katika Kiswahili Sanifu kuliitajirisha lugha hii kwa kuwa tafsiri hizi zilikiwezesha Kiswahili kuundiwa maneno aina nyingi kutokana na uwezo wake wa kunyumbuka.

Kutokana na juhudi za wasanifishajiwa Kiswahili, lugha hii iliunda msamiati mpya na pia ikakopa pale ilipolazimu ili kuiwezesha kwenda sambamba na maendeleo ya ulimwengu. Ingawa kabla ya kusanifishwa kwa Kiswahili Kiunguja kilikuwa kikikopa sana kiasi cha kuweza kubandikwa jina la 'Kiswahili kijingajinga'¹³ kama tulivyo kwisha sema, sasa kulikuwa na utaratibu maalumu uliofuatwa katika kukopa. Kama tulivyosema juhudi zilizofanywa zililenga katika kukikuza Kiswahili

katika misingi ya lugha za Kibantu. Wasanifishaji hawa pia walirekebisha hali ya ukopaji uliokuwa ume-fanywa zamani kiasi kwamba waliyachukua maneno ya kigeni na kuyapurura mpaka wakayatoa uasili wake wa kigeni na halafu wakayaingiza katika utaratibu wa lugha ya Kiswahili. Ndiposa maneno ya kigeni yafuatayo yakaingizwa katika Kiswahili kwa utaratibu wa kuendelezwa kama maneno yenye asili ya Kiswahili:

Kheri (Kiarabu) ---- Heri (Kiswahili)

Vinho (Kireno) ---- Mvinyo (Kiswahili)

Schule (Kijerumani) ---- Shule (Kiswahili)

Kukisanifisha Kiswahili kumesaidia sana isimu ya lugha hii. Hii ni kwa sababu baada ya kuchaguliwa kwa Kiunguja kuwa msingi wa kukisanifishia Kiswahili kulikuwa na mwendelezo mmoja wa maneno kimatamshi na kimaandishi. Sasa hali ya vurugu na mvutano iliyo-kuweko hasa baina ya Kiswahili kilichotetewa na Krapf (Kimvita) na kile kilichotetewa na Steere (Kiunguja) ilifutwa. Wakati huu, idadi kamili ya vokali na konsonanti za Kiswahili iliwekwa, na haikosi ni kutokea wakati huu mantiki na sheria tuzijuazo kuhusu lugha hii zilipoanza kubuniwa na kusemwa kuwa ni za Kiswahili.

Usanifishaji wa Kiswahili ulikuwa na manufaa mengine, nayo yanafungamana na kufunzwa na kufunziwa lugha hii mashuleni. Haja ya kusanifishwa kwa

Kiswahili kulikuwa na maana kuwa ufundishaji wake ungeongezeka na hivi ndivyo mambo yalivyokuwa. Hivi Kiswahili kiliweza kuenezwa na kukuzwa zaidi kwa kuwafikia watu wengi zaidi. Hususa, Kiswahili kilikuzwa ili kiweze kutosheleza haja za elimu maana baada ya mtu kupata elimu angeitumia katika nyanja nyingine mbalimbali.

Usanifishaji wa Kiswahili, bila shaka, ulifanywa mengi katika kukikuza na kukiendeleza Kiswahili pamoja na kukipa sura mpya. Hususa, jambo la kusisitiza hapa ni kwamba ni kutokana na juhudi za usanifishaji wa Kiswahili ndiyo Chuo cha Uchunguzi wa Lugha ya Kiswahili na Shirika la Fasihi la Afrika Mashiriki yakaanzishwa. Hivi leo mashirika haya yanashughulikia utoaji wa vitabu ingawa Chuo cha Uchunguzi wa Lugha ya Kiswahili kinashughulika na uchunguzi pia.¹⁴ Vitabu vinavyotolewa ni vya Kiswahili na vile vile uchunguzi unaofanywa ni kuhusiana na lugha ya Kiswahili na kwa hivyo mashirika haya yanasaidia katika ukuzaji wa Kiswahili.

2.5 HITIMISHO

Ingawa kutokana na usanifishaji wa Kiswahili watu walipata fursa ya kuwasiliana vema na taratibu wakaanza kuelewana, Kiswahili hakikupokelewa kwa

nguvu sawa kote Afrika Mashariki na kati. Isitoshe, siasa ya wakoloni ilikuwa ni ile iliyolenga katika kuwagawanya Waafrika na kuwatawala. Kwa sababu hii tunaweza kusema kuwa wakoloni walikosa ilhamu ya kuhimiza matumizi mamoja ya Kiswahili kwa dhati kwani walihofu kitendo hiki kingalikuwa ni cha kuuhatarisha utawala wao. Haikosi ni kwa sababu hii ndiyo watawala wa Afrika Mashariki na kati hawakuwa na sera yoyote madhubuti kuhusiana na lugha ya Kiswahili. Katika hali kama hii si mno kupata lugha ikiwa inakua na kwa hivyo ikiwa Kiswahili kilizidi kukua katika enzi hii kama tulivyokwisha ona, basi kilijilazimisha tu kwa kuwa mkondo ulikuwa umewekwa wazi na usanifishaji ulioanzishwa mnamo mwaka 1930.

Hapa tuna maana kwamba usanifishaji wa kiswahili uliweka tu misingi ya ukuzaji wa lugha hii na kisha hapakuwa na juhudi nyingi za kuikuza lugha hii. Hali hii iliondoshwa baada ya nchiza Afrika Mashariki kujipatia uhuru maana juhudi za ukuzaji wa Kiswahili zilianza upya na kwa moyo wa kupenda kama roho kwa kiumbe. Kiswahili, kwa mfano, kilifanywa lugha ya taifa Tanganyika punde tu baada ya Uhuru wa nchi hiyo. Halafu mikutano ya kimataifa kuhusu ukuzaji na uimari-shaji wa Kiswahili kama lugha ya kimataifa ikaanza kwa wingi huku ikijadili mambo mbalimbali kuhusiana na lugha hii. Kwa mfano, mwakani 1978 kulikuwa na

mkutano Burundi ambao ulishughulikia Istilahi za Fasihi. Halafu kuna juhudi nyingine kuhusiana na ukuzaji wa Kiswahili ambazo zinafanywa mumo kwa mumo Afrika Mashariki kwa mfano kuunda vyama vya Kiswahili kiwilaya, kimkoa n.k. Ni juhudi hizi za kutaka kuifanya lugha ya Kiswahili iweze kusahilisha mawasiliano katika ulimwengu wa sasa tutakazoshughulikia katika sura inayofuata.

2.6 TANBIHI

1. Lyons, John (1970) - New Horizons in Linguistics, uk. 19. (Tafsiri yetu)
2. Wamanga ni Waarabu kutoka Omani ambao waliwahi kuitawala Afrika Mashariki kabla ya kuja kwa wakoloni wa Kizungu katika karne ya 19.
3. Mkangi, K. katika makala yaitwayo Swahili Language and Culture na ambayo aliyatoa kwenye semina iliyokuwa The School of Oriental and African Studies, University of London: Aprili 1983, na ambayo yapatikana pia katika MWAMKO II - Jarida la Kiswahili Chuo Kikuu cha Nairobi, 1984, uk. 9.
4. Tazama Krapf, J.L. katika Utanguliziwa Kamusi yake ya Kiswahili (1882).
5. Chiraghdin, S. na Mnyampala M.E. katika Historia ya Kiswahili (1977) uk. 19.
6. Kapinga, M.C. (1983) - Sarufi Maumbo ya Kiswahili uk. xiii.
7. Kama 6 hapo juu
8. Kama 5 hapo juu lakini uk. 21
9. Nukuu hili tumelitoa katika KISWAHILI Vol. 35 - Makala yajulikanayo kama Swahili Language Policy yaliyoandikiwa na Wright, Marcia, kwenye uk. 48,

ambaye naye amelitoa katika "Note on the International Language Committee meeting Resolutions" katika Africa IV No.2 1931 uk. 240.

10. Nkwera F.V.M. - Sarufi na Fasihi Sekondari na Vyuo: uk. 123. Lakini neno 'lafudhi' limetumiwa visivyo. Lahaja ndilo neno mwafaka.
11. Tumetumia kifungu, 'Fasihi ya Kiswahili' tukiwa na maana ya kazi yoyote ya kifasihi ambayo imeandikwa katika lugha ya Kiswahili bila kujali mwandishi ni wa asili gani na imeandikwa katika mazingira gani.
12. Kama 6 hapo juu lakini uk. xv
13. 'Kiswahili kijingajinga' ni maneno aliyoyatumia Krapf ili kupinga kuwa Kiunguja ni lahaja safi ya Kiswahili. Alikuwa hivi kwa sababu kilikuwa kimekopa maneno mengi sana kutoka lugha za kigeni kiasi kwamba ule uasili wake ulikuwa haupo tena.
14. Tazama Mwangomango, J.S.: Kiswahili karne ya 20 katika Kiswahili vol. 42 uk. 14

SURA YA TATU

3.0 UKUZAJI WA KISWAHILI BAADA YA UHURU

3.1 UTANGULIZI

Wakoloni wa Kiingereza walifahamu umuhimu wa Kiswahili katika Afrika Mashariki lakini hawakufanya jitihada nyingi kukistawisha na kukipa mahali pake halisi. Ni kwa sababu hii ndiyo kukawa na shule chache sana wakati wa utawala wa Mwingereza na hata katika shule hizo ni Kiingereza kilichotiliwa mkazo kiasi kwamba mtu yeyote katika jamii aliyekimudu Kiingereza alikuwa na hadhi kuu na alihesabiwa miongoni mwa wale walioelimika na kustaarabika. Kwa sababu hii wananchi fulani walifanywa kuabudu Kiingereza huku wakikidharau Kiswahili na hili lingali katika fikira za baadhi ya wazee katika jamii zetu maana siku moja tulipomweleza mzee mmoja kijijini mwetu kuwa kwasoma Kiswahili katika chuo kikuu alituuliza kwa nini hatungechagua Kiingereza, badala ya Kiswahili ambacho chajulikana na kila mtu. Hali ya watu kuwaona wale walio na ujuzi wa Kiingereza kuwa bora kuliko wengine katika jamii ilizalisha makundi mawili ya watu miongoni mwa Waafrika nayo ni: la wenye elimu, waliokizungumza Kiingereza, na la "wajinga", wasio na elimu kwa kutokijua Kiingereza. Halafu wengi wa wale wenye elimu walikosa imani katika tamaduni za Waafrika. (Rejelea Lema, A. Katika Mulika Na. 2 uk. 3-4).

Lakini baada ya uhuru viongozi wa Afrika Mashariki walianza upya kuzizingatia na kuzistawisha tamaduni hizi za Waafrika. Haikosi ni kutokana na hali hii ndiyo Kiswahili nchini Kenya na Tanzania kikawa kinashughulikiwa ili kukistawisha kusudi kiwe lugha ya kujitosheleza na ya kujivunia.

Haja yetu hapa ni kujadili yaliyofanywa katika kuikuza lugha ya Kiswahili baada ya nchi za Afrika Mashariki kujipatia uhuru. Nyanja tutakazojadili ni pamoja na vyombo vya habari, maandishi, shule, taasisi na vyuo,, na warsha za ukuzaji na uendelezaji wa Kiswahili.

3.2 VYOMBO VYA HABARI NA UKUZAJI WA KISWAHILI

Katika kuikuza lugha, vyombo vifuatavyo vina umuhimu mkubwa sana: Magazeti, redio, televisheni, majarida, vitabu na maandishi yoyote yale. Ni vipi ambavyo vyombo hivi vya habari vimesaidia katika ukuzaji wa Kiswahili toka nchi za Afrika Mashariki zilipojipatia Uhuru?

3.21 MAGAZETI

Katika utangulizi wa sura hii tumesema kuwa baada ya nchi za Afrika Mashariki kujipatia uhuru viongozi wake walidhamiria kuzizingatia na kuzistawisha tamaduni za Waafrika. Lugha ni kipengee

mojawapo ya vipengee vya utamaduni. Halafu Khatibu, M.S. (1983:44) asema kuwa magazeti ni vyombo muhimu katika kuandaa umma ili kufuata mtazamo na mwelekeo mtawala anataka. Basi twatarajia kuwa magazeti ya Kiswahili yametumiwa (na yanatumiwa) katika kukikuza Kiswahili.

Siyo wananchi wengi katika Afrika Mashariki ambao wanakijua Kiingereza: kwa hivyo siyo wananchi wengi ambao wanaweza kuyasoma magazeti ya Kiingereza. Kwa bahati nzuri, wananchi wengi wa Afrika Mashariki wakiwemo wale walioachia masomo darasa la saba au hata chini yake na wale waendao katika madarasa ya kisomo cha watu wazima, wanajua kukisoma na hata kukiandikia Kiswahili. (Kwa ushahindi kuhusu hoja kuwa wale waendao katika madarasa ya kisomo cha watu wazima wanajua kusoma Kiswahili, Sikiliza kipindi cha Sauti kipindi cha Sauti ya Kenya Redio kiitwacho Maendeleo Wilayani.) Tunachotaka kusema hapa ni kwamba katika kuyasoma magazeti ya Kiswahili, wananchi wengi hujiongezea ujuzi wao wa Kiswahili kwa kuwa matumizi ya lugha katika magazeti haya huonyesha jinsi lugha hii inavyokua kila uchao. Hii ni kwa sababu ukilinganisha gazeti la Kiswahili lilokuweco mara tu baada ya uhuru kupatikana na yale yaandikwayo sasa utaiona tofauti kubwa sana kilugha. Kwa mfano katika magazeti ya siku hizi utakuta maneno kama ukimwi, tonoradi n.k.

ambayo hata ukitafutaje huwezi kuyapata katika magazeti yalioyoandikwa miaka kumi iliyopita. Yaani lugha ya sasa katika magazeti ina wingi wa upya wa dhana na istilahi za Kisasa. Basi magazeti ya Kiswahili yanaponunuliwa na kusomwa huwa ni kifaa muhimu cha kuikuzia lugha ya Kiswahili.

Magazeti ya Kiswahili, kama yalivyo magazeti ya Kiingereza, yana kurasa maalum zilizotengwa kwa wasomaji wake kutoa maoni yao ama kwa maandishi ya nathari au kishairi. Wahariri wa magazeti haya hawakikubali chochote kilichoandikwa; lazima kiwe kimeandikwa kwa lugha fasaha, na pale ambapo hakijaandikwa kwa lugha nzuri wahariri hukirekebisha kabla ya kukichapisha magazetini. Katika hali kama hii maandishi wa maoni magazetini hukuza Kiswahili kwa njia kadhaa. Kwanza, maandishi wa maoni magazetini hubidiishwa kuifanyia lugha yao utafiti na uchujaji wa kutosha ili iwe sanifu na ya kifasaha kusudi maoni yao yapate kuchapishwa mara tu yanapokelewa. Watu wasomao maoni kama haya hufaidi kwa upande wa ujumbe na lugha. Pili, pale wanapokosolewa na wahariri, maandishi hujua makosa yao na wanapoandika mara nyingine huandika kwa uangalifu mkubwa mpaka mwishowe wakajitokeza na Kiswahili safi. Halafu kutengewa kurasa magazetini ili kutoa maoni juu ya mada

mbalimbali huwapa wananchi kitu cha kujivunia kilugha na hivi wao hufanywa kuipenda lugha hii ya Kiswahili. Kwa sababu ya kuipenda, wao huanza kuitumia, japo kimakosa hapa na pale, na baada ya muda hujikuta wameongeza ujuzi wao wa Kiswahili.

Katika magazeti ya Kiswahili mara kwa mara hujitokeza uchambuzi wa vitabu mbalimbali vya Kiswahili. Vingi vya vitabu hivi huwa ni vile vinavyotahiniwa mashuleni katika somo la Fasihi ya Kiswahili. Kwa sababu hii watu wengi, wanafunzi kwa walimu pamoja na wapenzi wa lugha ya Kiswahili kwa jumla, hujinunulia magazeti wakitaka kujisomea uchambuzi uliofanywa na kuona ikiwa wanaafikiana nao au la. Kwa mfano mwaka jana (1987) Amutala alipokichambua kitabu cha Hussein, E. kiitwacho Mashetani katika Kenya Leo walimu pamoja na wanafunzi wengi wa Kiswahili walijisomea uchambuzi huo na twakumbuka wanafunzi wa shule fulani mkoani Nairobi kutuuliza kuwa mchambuzi alikuwa na maana gani katika kusema Shetani ni Mkoloni.

Katika kufanya uchambuzi wa vitabu magazetini hivi, wote (waandishi kwa wasomaji) husaidia katika kukukuza Kiswahili kwa kuwa huwatia watu wengine moyo wa kuyasoma maandishi yao na kuyajua maoni yao na kuyatathmini hasa pale mchambuzi wa kitabu anapokosolewa na wasomaji.

Isitoshe, katika magazeti ya Kiswahili mara kwa mara hutokeza makala kuhusu wanawake na pia sinema. Kuna watu katika jamii ambao watanunua gazeti kwa sababu ya kutaka kuona yaliyoandikwa kuhusu mwanamke fulani au kwa sababu ya kutaka kujua ni sinema gani inaonyeshwa wapi. Baada ya kutekeleza kusudi lao, watu kama hawa wanaweza kulisoma gazeti au mtu mwingine awapitie na kisha wampe gazeti hilo. Katika hali kama hii kuna uwezekano gazeti moja likazunguka miongoni mwa watu wengi na hivi watalisoma. Katika harakati za kulisoma gazeti hivi, wasomaji hujikuzia ujuzi wao wa Kiswahili.

3.22 REDIO NA TELEVISHENI

Redio na televisheni ni vyombo muhimu sana ambavyo vimesaidia katika kukieneza na kukikuza Kiswahili. Mwelekeo wa utangazaji ambao hutumiwa katika Afrika Mashariki umekuwa ni nyenzo muhimu ya kukikuza Kiswahili kote ulimwenguni kwa kuwa kila idhaa ya Kiswahili ulimwenguni hujaribu kuiga Kiswahili kitangaziwaqho katika nchi za Afrika Mashariki. Kwa mfano, ukiifungulia idhaa ya Kiswahili yoyote utagundua kuwa karibu idhaa zote, isipokuwa labda idhaa ya Kiswahili ya Redio Zaire pekee, zinatumia Kiswahili kama kile kitumikacho katika Redio Tanzania, Redio Uganda na idhaa ^{ya Kiswahili} ya Sauti ya Kenya. Labda sababu kuu za hali hii ni kwamba Kiswahili kina chimbuko lake katika Afrika Mashariki,

na pia kuwa juhudi nyingi za kukikuza Kiswahili zafanywa humo. Kwa mfano, kabla ya kuja kwa jina 'Ukimwi' kwa maana ya 'Aids' idhaa nyingi zilikuwa zikitumia 'Aids' tu lakini zilipolisikia latumika Kenya na Tanzania idhaa nyingine zimelichukua na kuanza kulitumia kiasi kwamba hivi sasa 'Ukimwi' limeshika kama Kiswahili cha 'Aids.'

Utangazaji pia una umuhimu mwingine katika kuikuza lugha ya Kiswahili. Katika kutangaza ni lahaja sanifu ya lugha itumiwayo na kwa hivyo watangazaji hufanya vyo vyote vile kuitumia lugha sanifu hususa katika kutangaza habari muhimu kama Taarifa ya habari, Mazungumzo baada ya habari n.k. Huku kutumia lugha sanifu huwaathiri watumiaji wa Kiswahili hasa wale watumiao Kiswahili cha kilahaja hata wakatambua kuwa kumbe wanavyoongea Kiswahili wao sivyo kinavyoongewa kwingi. Basi kupitia kwa utangazaji redioni na kwenye televisheni watu hujibidiisha kuzungumza Kiswahili Sanifu ili waeleweke kote.

Katika vipindi vya redio kama vile Chaguo lako mahojiano (Kenya) na Jioni njema (Tanzania), wananchi hupewa fursa ya kuwapelekea jamaa na marafiki salamu pamoja na jumbe ambazo huwa, mara nyingi, ni tafsiri kutoka kwa lugha za kwanza za wale wanaopeleka salaam na jumbe. Hii ni njia moja ya kuitajirisha lugha

ya Kiswahili, na ni huku kuitajirisha lugha kunakoitwa kuikuza lugha hasa.

Redio na televisheni huwa na vipindi ambavyo baadhi ni muhimu sana katika ujuzaji wa Kiswahili. Badala ya kuwatumia walimu madarasani tu, mafunzo ya Kiswahili (Lugha na Fasihi) hutolewa redioni. Isitoshe, redioni kuna baadhi ya vipindi ambavyo vimelengwa katika kuwawekea wazi watumiaji wa Kiswahili maneno na dhana pamoja na istilahi ambazo huenda wakazona kuwa ni ngumu. Kwa mfano kipindi cha Mbinu za Kiswahili (Tanzania) na cha Lugha Yetu (Kenya) husaidia sana katika ukuzaji wa Kiswahili kwa kuwa huwashirikisha mabingwa wa lugha na isimu ya Kiswahili kiasi kwamba baada ya kukubaliana juu ya jambo fulani umma hulichukua na kuanza kulitumia mara moja kwa kuwa wananchi wana imani na hawa mabingwa wa Kiswahili.

3.3 WAANDISHI WA VITABU

Waandishi wa vitabu vya Kiswahili wamesaidia na wanaendelea kusaidia katika harakati za kuikuza lugha hii. Waandishi wa vitabu hufanya utafiti wa kutosha kabla hawajaandika chochote kwani huwa wakichelea kazi zao zisije zikabezwa. Utafiti ufanywao na waandishi wa vitabu vya Kiswahili, kama ulivyo wa waandishi wa vitabu vya lugha nyingine, huhusu

misamiati, maandishi bora, vitabu vya sarufi, fasihi na makamusi. Linaloonekana hapa ni kwamba waandishi wa vitabu hufanya kila linalobidi ili kuona kuwa lugha inatekeleza haja ya kuwasiliana kijamii na kitaalamu.

2.31 VITABU VYA FASIHI

Mwandishi wa vitabu vya fasihi hajifungi katika lugha hiyo anayoiandikia. Yeye hutamba katika lahaja zote za lugha anayoiandikia kitabu chake na akishindwa kulipata neno mwafaka kwa kile anachotaka kusema hujitosa katika lugha jirani zilizo za nasaba moja na ile anayoiandikia. Hili likishindwa, mwandishi wa fasihi ana uhuru wa kuchukua neno la lugha yoyote mradi lilete maana ile aliyoikusudia. Ikiwa juhudi zote hizi zitashindwa kumpa mwandishi wa vitabu vya fasihi neno mwafaka, basi ana uhuru wa kujiundia neno lake mwenyewe. (Tazama neno 'Tirivyogo' ambalo limeundwa na Mohamed Suleiman Mohamed katika Nyota ya Rehema).

Kama inavyoonekana kutokana na maelezo yaliyo hapo juu, mwandishi wa vitabu vya fasihi, hasa pale anapoandikia maudhui yavutiayo wengi, ni mkuzaji mkubwa wa lugha kwa jinsi alivyo na uhuru wa kuzua neno na akalिसambaza kwingi likapata kutumiwa na

kushika miongoni mwa watu wengi. Hali hii huendelezwa kwa kasi zaidi ikiwa vitabu hivyo vilivyoandikwa vitatahiniwa mashuleni katika somo la Fasihi. Kwa kuwa Fasihi ya Kiswahili sasa ina waandishi wengi, inasaidia kukikua Kiswahili.

Pia, tafsiri ziingizwazo katika Fasihi ya Kiswahili husaidia katika kuikua lugha hii. Ikumbukwe kuwa vitabu vingi vitafsiriwavyo kwa Kiswahili aghalabu huwa vimeandikwa kwa Kiingereza kwanza. Kwa kuwa idadi 'nzuri' ya watu wanakijua Kiingereza, wanaposoma neno fulani katika tafsiri za vitabu vilivyo katika Kiswahili hujuzwa kuwa Kiswahili cha neno fulani la Kiingereza ni hiki. Kwa mfano, tafsiri ya The Merchants of Venice iliyofanywa na Nyerere, J.K. badala ya kuwa ni wafanyibiashara wa Venisi imekuwa ni Mabepari wa Venisi. Yaani Nyerere katika tafsiri hii yake amewatanabahisha watumiaji wa Kiswahili kuwa 'Wafanyibiashara' ni neno la kawaida mno.

3.32 VITABU VYA SARUFI

Kabla ya kupatikana kwa uhuru vitabu vingi vya sarufi viliandikwa na wageni. Pia waliandika vingi vya vitabu hivi katika lugha ya Kiingereza. Baadhi ya wageni hawa walipotisha Kiswahili kwa kukiendeleza visivyo. Kwa mfano, methali ya Kiingereza 'Blood is thicker than water' ilipewa tafsiri na fasiri ya moja kwa moja isemayo 'Damu nzito kuliko maji' badala ya 'Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe'.

Kwa bahati nzuri, baada ya kupatikana kwa uhuru wananchi wa Afrika Mashariki wamejitokeza na kuandika vitabu vya sarufi ya Kiswahili na kwa Kiswahili kitupu. Kazi za akina Kapinga, M.C, Kabugi, C., Mbaabu, I., Nkwera, F.V.M. n.k. ambazo zimeandikwa kwa Kiswahili zinasaidia sana katika kukikuza Kiswahili maana hapana kusumbuka tena kutafutia maneno ya Kiingereza visawe vyake katika Kiswahili.

Isitoshe, katika vitabu vya sarufi kama hivi mna sheria mbalimbali kuhusu lugha. Kwa kutumia sheria hizi kikamilifu na kibusara tunaweza kuikuza lugha ya Kiswahili kwa kutumia kila kiungo chake kifaapo ili kuyasahilisha mawasiliano. Pia tunatumia sheria hizi za sarufi ili kuipanua lugha ya Kiswahili kimsamiati. Kapinga, M.C. katika Sarufi Maumbo ya Kiswahili (1983) asema kuwa Kiswahili, kama lugha nyingine za Kibantu, kina tabia ya kunyumbuka. Ni kutokanana sheria hii ndiyo maneno kama 'Boresha' kutokana na sifa 'Bora' au 'Maskinisha' kutokana na sifa 'Maskini' yanaingizwa katika Kiswahili ili kukitajirisha kimsamiati.

3.33 MAKAMUSI

Makamusi ya Kiswahili ni mengi.¹ Katika kujadili mada yetu ya utafiti tutatumia Kamusi ya Kiswahili Sanifu (1981) na Kamusi ya Tiba² kama vielelezo vya makamusi

ambayo yanasaidia katika ukuzaji wa Kiswahili.

Kwa sababu ya maendeleo ulimwenguni miktadha mingi ya lugha inaingiza istilahi na dhana nyingi ngeni katika lugha. Istilahi na dhana hizi ngeni wakati mwingine huwatatanisha watumiaji na wapenzi wa lugha fulani. Ni kwa sababu hii ndiyo Wanaisimu huandika makamusi ili kutumia lugha kuelezea lugha.

Kwa matumizi ya haraka, makamusi haya ya Kiswahili yameandikwa kwa mpango fulani nao ni kwamba maneno yake yamepangwa ki-alfabeti. Sababu ya hili ni kwamba ukitaka kupata maana ya neno kama 'Chambenga' ambalo umelisikia kwa mara ya kwanza mahali fulani unafunua kamusi pale palipo na maneno yaanzayo kwa [tʃ]. Hivi utapata maana ya neno hilo bila kusumbuliwa kwa kutafuta sana kiasi cha kuweza kukata tamaa.

Pia, ili kumsaidia msomaji wa makamusi haya katika kukikuza Kiswahili chake, kila neno limefafanuliwa badala ya kuliwekea mishabaha tu bila ya ufafanuzi na kumdhania msomaji kuwa analielewa neno fulani na matumizi yake mbalimbali.³ Hili lina manufaa ya kukikuza Kiswahili maana si rahisi kumpotosha mtumiaji wa neno fulani kutokana na ufafanuzi mwema ambao makamusi haya hutoa.

Makamusi haya yana umuhimu mwingine kwa mwanafunzi wa Kiswahili. Kabla ya kutoa ufafanuzi wa neno au kisawe chake, makamusi haya yanaeleza neno hilo ni sehemu gani ya usemi⁴ pamoja na kueleza data nyingine za Sarufi.

Ni dhahiri kwamba makamusi haya yana umuhimu mkubwa katika ukuzaji wa Kiswahili maana katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu (1981) tunaambiwa kuwa

Katika kamusi hii idadi ya maneno imekuwa kubwa kuliko katika kamusi zilizotangulia. Kuzidi kwa idadi ya maneno kunaonyesha maendeleo ya lugha.⁵

Linalojitokeza kutokana na nukuu hili ni kwamba makamusi ni vifaa vya kupimia maendeleo ya lugha na Kamusi ya Kiswahili Sanifu (1981) inaonyesha maendeleo ya Kiswahili.

3.4 SHULE, TAASISI NA VYUO

Nchini Tanzania Kiswahili chatumika kwingi sana katika ufundishaji. Kwa mfano, katika shule za msingi karibu masomo yote hufunzwa katika Kiswahili na katika shule za sekondari somo la Siasa pamoja na Lugha na Fasihi ya Kiswahili hufunzwa katika Kiswahili. Nchini Kenya mambo yamekuwa ni kinyume kwa kuwa Kiswahili kimekuwa hakitiliwi mkazo sana hasa katika shule za

msingi, lakini uanzishaji wa mfumo mpya wa elimu ya 8:4:4 ambao umekifanya Kiswahili somo la lazima katika mtihani wa shule za msingi na pia wa shule za sekondari, bila shaka, utakiimarisha Kiswahili nchini humu. Huku kufunzwa Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za msingi na zile za sekondari kunakuza Kiswahili kwa kuwa kunaiimarisha lugha hii katika madarasa ambapo kuna idadi kubwa zaidi ya wanafunzi. Huku kuwafunza wanafunzi hawa Kiswahili huwaandaa kuwa wataalamu wa lugha hii siku zijazo. Mathalani, endapo watafanikiwa kuwa walimu wataisambaza na kuikuza lugha hii hata zaidi.

Katika kuandaliwa kwa kazi kama ya ualimu au kuwa wataalamu wa Kiswahili, licha ya kufunzwa Kiswahili, wanafunzi pia hushajiishwa na walimu wao kuunda vyama mbalimbali ambavyo hujishughulisha na uimarishaji wa lugha hii. Katika shule nyingi kuna Chama cha Mijadala ambapo vichwa mbalimbali hujadiliwa, na hali hii huwapa wanafunzi fursa ya kujijenga kama wazungumzaji wa hadharani kwa Kiswahili. Mashindano pia huandaliwa na walimu ili wanafunzi wa shule mbalimbali wapimane nguvu katika nyanja kama vile usomaji, mazungumzo ya ghafla, ukariri wa mashairi n.k. Mashindano haya hukuza Kiswahili fasahamiongoni mwa wanafunzi huku yakizuia kadiri iwezekanavyo matumizi yake mabaya.

Katika Afrika Mashariki kuna taasisi kadhaa. Jukumu kubwa la baadhi ya taasisi hizi ni utunzaji na uimarishaji wa lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, baadhi ya taasisi hizi zimelisahau jukumu hili na tuna-weza hata kusema kuwa ziko kwa jina tu. Taasisi inayoikuza lugha ya Kiswahili kikweli ni Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Wanataasisi hii wamefanya mengi hasa katika uwanja wa istilahi za Fasihi ya Kiswahili na haya wamefanya kwa kujadili zile istilahi zilizo katika Kiingereza na kisha kuzitafutia visawe vyaka katika Kiswahili. Majarida maarufu yatumikayo kote ulimwenguni kunakofunzwa Kiswahili: Kiswahili na Mulika ni kutokana na jasho na bidii za Wanataasisi hii.

Kamusi ya Kiswahili Sanifu (1981) ni zao jingine la juhudi za Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Hakika bila ya kuwa na kamusi hii viwango vya ujuzi wa Kiswahili kwa wengi wetu vingekuwa vya hali ya chini sana. Mbali na kamusi hii, wanataasisi pia hukuza Kiswahili kwa juhudi zao za kujadili msamiati wa fani mbalimbali katika semina na kongamano mbalimbali. Baada ya kujadili msamiati hivi, wao huandika katika majarida tuli-yoyataja hapo juu na kisha wakayauza kwa wapenzi wa Kiswahili kote ulimwenguni.

Vyuo pia ni vyombo muhimu vya ukuzaji na uimarishaji wa lugha. Licha ya kuwa na vyuo vinavyotoa Vyeti na Diploma kwa walimu wafunzao Kiswahili, kuna Vyuo Vikuu katika Afrika Mashariki ambavyo huzalisha walimu pamoja na wataalamu wa Kiswahili ambao wote huisaidia lugha ya Kiswahili katika kukua kwake. Katika vyuo hivi kunafunzwa Fasihi ya Kiswahili na Matumizi ya Lugha ya Kiswahili ukiwemo ustadi wa lugha, isimu ya lugha, n.k. katika Kiswahili. Juhudi hizi za vyuo hutayarisha walimu wenye ujuzi katika Kiswahili na wao mara nyingi huenda kufundisha Kiswahili katika shule za msingi, za sekondari na vyuo vingine kunakofunzwa Kiswahili ili kuwapa wanafunzi misingi miema ya lugha hii kinyume na enzi ya ukoloni wa Mwingereza Kiswahili kilipokuwa kikifunzwa na walimu ambao baadhi walikuwa na ujuzi hafifu wa lugha hii.

Isitoshe, katika vyuo hivi, na hasa katika vyuo vikuu, kuna utafiti mwingi ufanywao kuhusiana na Kiswahili na kwa kuwa mwingi wa utafiti huu huwa ukifanywa kwa madhumuniya kutahiniwa kama kazi ya kumwezesha mtu kuipata shahada yake watafiti hujitokeza na matokeo yenye mashiko ambayo husaidia katika ukuzaji wa Kiswahili hasa pale ambapo mada ya utafiti yahusu Isimutumikizi.⁶

3.5 SEMINA ZA UKUZAJI WA KISWAHILI

Kumekuwa na semina/warsha kadhaa katika Afrika Mashariki na Kati na ambazo zimekuwa na lengo la kuishughulikia lugha ya Kiswahili ili kuitajirisha kimsamiati kwa kuiundia istilahi. Semina za aina hii zilianza mwaka 1978 huko Burundi na baada ya mwaka huo zikafuata nyingine kadhaa, zote zikiwa na lengo lile lile la kukikuza na kukimarisha Kiswahili. Semina hizi zote zimefanya mengi katika nyanja hii lakini, kwa maoni yetu, ni semina mbili zilizo na umuhimu mkubwa zaidi ya zote katika ukuzaji wa Kiswahili ili kukiwezesha kuyakabili mabadiliko na maendeleo ya kisayansi na ya kiteknolojia yaliyoko sasa. Semina hizi mbili ni ile iliyofanyika mwezi Novemba 1986 pale Tanzania Bureau of Standards na ya mwezi April/Mei 1987 iliyofanyika Kiswahili Building, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kwa kuwa semina ya 1986 ndiyo iliyolazimisha kuwoko kwa ile ya 1987, tutaizungumzia tu ile ya 1987 na mafanikio pamoja na kasoro zake kuhusiana na ukuzaji wa Kiswahili.

Semina hii ya 1987 ilishughulikia istilahi za Isimu na Lugha, Kemia, Fizikia pamoja na Biolojia na ilikuwa na washiriki kutoka Zaire, Rwanda, Burundi, Kenya, Uganda na Tanzania. Wataalamu katika kila taaluma ya hizo zilizoshughulikiwa waliushughulikiwa

uwanja wao huku wakiongozwa njia na Wanaisimu. Kabla ya kazi hii kuanza kulikuwa na kipindi cha kutayarisha miongozo na maagizo ambayo yangefuatwa katika kuishughulikia kazi hii. Baada ya kazi ya kujadili na kusanifisha istilahi hizo kuisha, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili ilizikusanya istilahi zote katika jarida moja na kuzipeleka kote kinakozungumzwa Kiswahili ili wapenzi pamoja na watumizi wa lugha hii kote ulimwenguni wapate kuzisoma, kuzitathmini na kuwapelekea Wanataasisi maoni yao kuhusu istilahi hizo.

Juhudi hizi zilikuwa na athari fulani nzuri kuhusu ukuzaji wa Kiswahili. Kwanza, kuwa na washiriki kutoka kote Afrika Mashariki na kati kuna maana kuwa hapakuwa na ubinafsi wa nchi moja katika harakati hizi za kusanifisha istilahi za nyanja tulizozitaja hapo juu. Yaani wote walitaka kukikuza Kiswahili kama lugha moja. Na kushirikishwa kwa wataalamu wa taaluma mbalimbali katika shughuli hii ya wanaisimu kulisaidia kupata mipaka baina ya mambo madogo madogo ambayo wanaisimu pekee labda wasingeyatambua kwa urahisi. Hata wanaisimu pia walichuguliwa kusimamia nyanja mbalimbali si tu kwa kuwa wao ni wanaisimu bali pia kutegemea tajriba zao katika nyanja hizo. Kwa mfano Mkude, D.J. kwa sababu ya ujuzi wake wa

miaka mingi katika isimu alikuwa Mwenyekiti wa kamati iliyoshughulikia isimu, na Kitsao, J. kwa sababu ya kushiriki kwake katika utayarishaji wa Kamusi ya Tiba, Chuo Kikuu cha Nairobi, alipewa uwenyekiti wa kamati iliyoshughulikia istilahi za Biolojia kwa kufungamana kwa Biolojia na mambo ya tiba. Hali hizi zote zaonyesha kuwa istilahi zilizopatikana zilikuwa madhubuti kwa kuwa kazi ya kuzizalisha ilifanywa kwa dhati na kwa makini makubwa.

Isitoshe, kule kutayarisha miongozo ambayo ingefuatwa katika kuishughulikia kazi ya usanifishaji wa istilahi kwaonyesha kuwa misingi fulani iliwekwa na wanaisimu na ilifuatwa kote ili kujitokeza na kazi mwafaka. Misingi hii iliyowekwa ilijikita katika ule mfumo wa kimataifa uitwao ISO na kwa hivyo istilahi walizojitokeza nazo wale waliozishughulikia ni za kutumika kote ulimwenguni na wala si katika Afrika Mashariki na Kati pekee. Hii ndiyo maana istilahi hizo zote zikakusanywa katika jarida na kupelekewa mataifa yote yanayokitumia Kiswahili. Kitendo hiki cha kuzituma istilahi kote kinakotumiwa Kiswahili kuna maana kuwa wasanifishaji wa istilahi hizi walikuwa na uhakika na kile walichokuwa wamekifanya, na pia

walikuwa radhi kukosolewa ili pale palipoenda kombo parekebishwe kusudi Kiswahili kipate kukuzwa vema.

3.6 KASORO ZA JUHUDI HIZI ZA UKUZAJI WA KISWAHILI

Kutokana na haya ambayo tumeeleza hapo juu ni dhahiri kwamba baada ya wakoloni wa Kiingereza kudondoshwa na mahali pao kuchukuliwa na Waafrika wenyewe, juhudi nyingi zimefanywa ili kukikuza Kiswahili kulingana na mahitaji ya wakati wa baada ya uhuru. Lakini je, twaridhika na juhudi hizi?

Ni kweli kuwa magazeti ya Kiswahili ni mengi katika Afrika Mashariki lakini magazeti haya huwa hayajitokezi na habari au makala asilia. Yaani magazeti haya ni vimelea vya yale ya Kiingereza kwa kuwa unapolisoma gazeti la Kiswahili linaonekana moja kwa moja kuwa ni mwigo wa lile la Kiingereza (Mathalani tazama Taifa Leo na Daily Nation ya Kenya ya tarehe yo yote ile moja). Pia, magazeti ya Kiswahili huwa na habari chache na ambazo aghalabu huwa zimesomwa kitambo katika magazeti ya Kiingereza. Hapa tuna maana kuwa katika magazeti ya Kiswahili kuna uchujaji mwingi wa habari na ambazo hujitokeza kama tafsiri ya zile za magazeti ya Kiingereza. Hii ndiyo maana mara kwa mara huwasikia wasomaji wakilalamika kuwa tafsiri za habari na makala kama haya huwa zimepotoshwa kabisa.⁷

Tafsiri kama hizi hutweza ukuaji wa Kiswahili kwa kuwa mtu asiyekijua Kiingereza hawezi kupata maana iliyokusudiwa na makala asilia katika gazeti la Kiingereza, na hata yule anayekijua Kiingereza wakati mwingine hulazimika kurejelea makala asilia katika gazeti la Kiingereza. Kwa sababu hii, watu huona ni afadhali kujisomea magazeti ya Kiingereza kuliko kujisumbua kwa kuyasoma yale ya Kiswahili ambayo huwa yameandikwa na watu ambao ama hawajui nadharia ya tafsiri au hawazijui lugha zote mbili barabara.

Fauka ya haya, magazeti ya Kiswahili huwa na matangazo ya biashara machache sana licha ya sura nyingine za gazetini kama vile matangazo kuhusu sinema, makala kuhusu vitabu, wanawake n.k. kuwa haba. Je, ni nani atakayeyaacha magazeti ya Kiingereza yaliyo na sura hizi zote kwa ukamilifu wake ayanunue yale ya Kiswahili ambayo ni pungufu?

Kuhusu vitabu vya Kiswahili kuwa zana ya ukuzaji wa lugha hii, haturidhiki na hali ya mambo hususa nchini Kenya. Waandishi wengi wa vitabu vya Kiswahili huvandika vile vya shule tu maana wanafahamu soko i tayari. Wao huzisahau nyanja nyingine kama za Fasihi, Historia, Sayansi n.k. kana kwamba watu wote wanapotaka kusoma vitabu vya Kiswahili wavisome hivi vya shule. Tena ni vigumu sana kwa musuada wa kitabu

cha Kiswahili kukubaliwa na wachapishaji wa vitabu kwa kuwa wanaamini kuwa hapana soko kwa vitabu vya kiswahili nchini Kenya, kinyume na ilivyo nchini Tanzania na labda hii ndiyo sababu kitabu cha mashairi-huru hakijawahi kuandikwa na Mkenya ingawa mijadala kuhusu maendeleo ya ushairi katika Chuo Kikuu cha Nairobi yaonyesha kuwa ushairi huu unaungwa mkono na wengi. Isitoshe, nchini Kenya baada ya Kitabu fulani kuandikwa hata kikiwa ni kizuri kinachoweza kutahiniwa shuleni huwa hakipendekewi mara moja, au hata kwa kusomwa tu darasani si mno kupendekezwa. Hata pale kitabu fulani kinapopendekezwa kuwa kitahiniwe huwa kupatikana kwake ni vigumu. Pia, nchini Kenya hapana shirika madhubuti la waandishi wa vitabu vya Kiswahili kama ilivyo nchini Tanzania ambako kunalo. Ijapokuwa si nia yetu kupima Kenya na Tanzania katika mizani, kinachonekana ni kwamba Watanzania na juhudi zao huvifanya vitabu kuwa zana muhimu katika ukuzaji wa Kiswahili kuliko wafanyavyo Wakenya.

Ijapokuwa twatambua kazi muhimu inayotekelezwa na Kamusi ya Kiswahili Sanifu (1981), Kamusi hii pekee haitoshi kuikuzia lugha inayokua kwa kasi kama Kiswahili. Hii kamusi ni moja tu ilhali kuna nyanja

nyingi sana za kushughulikia. Kila taaluma yafaa iwe na kamusi yake na utayarishaji wa musuada wa Kamusi ya Tiba ni hatua inayopigwa kuelekea huko.

Kasoro nyingine inayoonekana katika kamusi hizi mbili tulizozirejelea kwa kazi yetu ni kuwa kamusi hizi zatoa kuendelezwa kwa maneno lakini hazifafanui jinsi maneno fulani kati ya maneno haya yanavyotamkwa. Hali hii kwa kiasi fulani hutweza Kiswahili kwa kuwa huenda pakatokea watu wengine wakatamka maneno jinsi wanavyofikiria wao, na hivi huenda wakaleta maana ambayo ni tofauti kabisa na ile iliyokusudiwa. Kwa mfano Mwingereza anayejifunza Kiswahili kwa kutumia kamusi hizi ana hatari ya kutamka neno 'Sharti' kama 'Shati' kwa sababu huenda akafuata mtindo wa kutamkwa kwa maneno ya Kiingereza. Yaani lazima kuwe na maandishi ya kifonetiki yatakuo tuwezesha kujua jinsi ya kutamka maneno. Kwa mfano ikiwa ni neno kama 'nge' likiandikwa mbele yake [ŋgɛ] itafaa zaidi kuliko pale yanapo andikwa na kuachwa tu kana kwamba watu wote wajua kuwa maneno ya Kiswahili hutamkwa jinsi yaandikwavyo.

Redio na televisheni kama vyombo muhimu vya ukuzaji wa Kiswahili wakati mwingine haviridhishi. Kuna makosa ya kisarufi yatokeayo mara kwa mara redioni na katika televisheni wakati wa matangazo kiasi kwamba wasikilizaji wanaweza kufanywa kuamini kuwa

hayo ni matumizi sahihi. Kwa mfano huwa tukiwasikia watangazaji wetu wakitumia maneno 'Jangili' na 'Jambazi' kana kwamba yana maana moja au maana inayoi-ngiliana ilhali kila moja lina mahali pake maalumu, sawa na maneno 'Mtaa' na 'Barabara.' Makosa haya hutokea kwa sababu ama watu wafanyao kazi ya kutafsiri hawaimudu kazi yao barabara, hali inayowafanya kuupotosha umma au kwa baadhi ya watangazaji kutojali tu makosa haya labda kwa kuyaona kuwa ni madogo sana.

Pia, wakati mwingine watangazaji hawa hawatambui kuwa wanayoyasema ni makosa. Kuikuza lugha hivi si kuikuza bali ni kuitweza.

Tumesema kuwa kipindi cha Lugha Yetu cha Idhaa ya Taifa ya Sauti ya Kenya kinasaidia katika ukuzaji wa Kiswahili. Lakini kipindi hiki hujadili mambo na yakaishia katika chumba cha kutangazia cha Sauti ya Kenya. Tunachosema hapa ni kwamba kutoka kipindi hiki kilipoanza kwa jina la Ubingwa wa Lugha mpaka kubadili jina na kuwa Lugha Yetu hapajatokea jarida au hata makala magazetini yenye maneno haya ambayo hujadiliwa. Juhudi za kipindi hiki zitakuwa na nguvu zaidi ikiwa jarida litatolewa baada ya muda fulani ili watu wajisomee maneno yaliyojadiliwa na kupendekezwa yatumike. Hii ni kwa sababu Wanalugha-yetu

wanapoyajadili maneno siyokila mpenzi wa Kiswahili huwa karibu na redio.

Ingawa warsha ya kusanifisha istilahi za lugha na Isimu, Kemia, Fizikia na Biolojia iliyofanyika Dar es Salaam mwaka 1986/87 ilifanya makubwa kuhusiana na ukuzaji wa Kiswahili, hapa na pale juhudi za warsha hii zaweza kuuliziwa maswali. Katika warsha hii ilipitishwa kuwa majina ya watu, nchi au miji yanapotumika, mashina ya majina hayo yahifadhiwe katika istilahi za Kiswahili. Kwa mfano.

Americium liwe Americi,
Lawrencium liwe Lawrenci,
Californium liwe Californi n.k.

Hatuna ugomvi na Californium kuwa Californi bali ugomvi wetu wahuu Americium kuwa Americi na Lawrencium kuwa Lawrenci. Ugomvi wenyewe wahuu jinsi ya kutamka istilahi hizi hasa tukizingatia kuwa kitamkwa 'C' hakijisimamii katika Kiswahili Sanifu. Je, hii Americi itatamkwa Ameriki, Americhi au Amerisi? Na katika kutamkwa tunavyohiari tutatumia vigezo gani?

Warsha hii ya mwaka 1986/87 ilichukua Ovari kuwa ndicho Kiswahili cha neno Ovary la kiingereza. Neno la Kiingereza Ovule lilipewa Ovule kama

Kiswahili chake. Hapa twatarajia kwamba ni sauti ambayo ingekopwa ili tupate Ovyulu lakini sivyo ilivyo. Isitoshe, tukitarajia kuwa utaratibu huu wa ukopaji ungeendelea hivi twapata Ovum la Kiingereza limepewa Yai kama Kiswahili chake badala ya Ovamu, na pia Ovipary badala ya kuwa Ovipari Kiswahili chake kimekuwa ni Utungaji. Hali kama hii inapotosha mtu anapotaka kutumia mantiki ya lugha katika kupata Kiswahili cha maneno kama haya. Maoni yetu ni kwamba katika majina ya jamii moja kama haya kupatiwa visawe vyake utaratibu mmoja sharti utumiwe.

Tumesema kuwa uanzishaji wa mfumo mpya wa elimu ya 8:4:4: nchini Kenya ni hatua kubwa iliyopigwa katika kutekeleza haja ya kukikuza na kukiimarisha Kiswahili. Lakini mfumo huu wa elimu una kasoro nayo ni kuwa umekuja kwa ghafla sana. Kabla ya kuanzishwa kwa mfumo huu, Kiswahili nchini Kenya kilikuwa hakitiliwi maanani katika baadhi ya shule za sekondari. Kiswahili kilipofanywa somo la lazima mashuleni hapakuwa na walimu wa kutosha waliokuwa wameandaliwa kukabiliana na hali hii. Kwa sababu hii walimu ambao wana misingi hafifu ya Kiswahili, wengi wao wakiwa ni wale wanaojua kukiongea tu, wamelazimishwa kukifunza. Katika hali kama hii mfumo huu wa elimu utazaa matunda aina gani Kilugha?

Halafu kuna vyuo, hasa vyuo vikuu, ambavyo vyatakikana vifunze walimu watakaofunza Kiswahili katika shule za msingi na za Sekondari pamoja na vyuo vingine lakini vyuo hivi pia vina matatizo yake. Kwa mfano, nchini Kenya kuna vyuo vikuu vinne ambavyo takribani vyote vyafunza Kiswahili lakini tatizo ni kuwa havina wahadhiri wa kutosha kuweza kuikabili idadi kubwa ya wanafunzi watakaokujifunza Kiswahili. Hapa tatizo si kwamba hapana wahadhiri wa kutosha nchini Kenya bali husemwa kuwa hakuna fedha za kuweza kuwalipa. Hali hii ya ukosefu au uhaba wa wahadhiri ina hatari ya kuzalisha walimu pamoja na wataalamu ambao hawakutathminiwa vilivyo, na ambao wanaweza kuwapotosha wanafunzi watakaofunzwa nao pale wanapoenda kufunza.

3.7 HITIMISHO

Ni dhahiri kwamba kwa kiasi fulani Kiswahili kimekuzwa sana na vyombo mbalimbali. Lakini kama ambavyo imedokezwa hapo juu, juhudi za vyombo hivi vya ukuzaji wa Kiswahili haziridhishi sana kwa kuteteleka hapa na pale. Basi katika sura ijayo, na ambayo ndiyo ya mwisho katika kuiangalia kazi yetu ya utafiti, mbali na mambo mengine tutatoa mapendekezo na maoni kuhusu njia bora za ukuzaji wa Kiswahili.

3.8 TANBIHI

1. Tunasema Makamusi ya Kiswahili ni mengi maana maelezo yetu ya Kamusi yamejikita katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu (1981) inayoeleza kamusi kuwa ni kitabu cha orodha ya maneno yaliyopangwa kwa mujibu wa alfabeti pamoja na maelezo yake. Basi tunachukulia vijitabu ambavyo watalii wajao Afrika Mashariki huonekana navyo kuwa ni makamusi.
2. Kamusi ya Tiba ambayo tumerejelea kwa kazi hii ni musuada ambao haujachapishwa bado. Kamusi hii imetayarishwa na Idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika Chuo Kikuu cha Nairobi.
3. Tazama Utangulizi wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu (1981) Uk. VII.
4. 'Sehemu za usemi' ni maneno katika lugha lakini ambayo yamevunjwawunjwa na kuwekwa katika mafungu mbalimbali. Kazi hii ya kuyaweka maneno katika mafungu hutekelezwa na Sarufi na ili neno kuwekwa katika fungu fulani itategemea ama kazi ya neno hilo katika sentensi au jinsi neno hilo linavyowasilisha ujumbe. Baadhi ya wataalamu akiwemo Profesa Mutahi wa Chuo Kikuu cha Nairobi huhiari kutumia istilahi 'Sehemu za kutamkia' au 'Ala za kutamkia' badala ya 'Sehemu za Usemi' kwa maana ya 'Parts of Speech'.

5. Kama Na. 3 hapo juu. .
6. Isimu - tumikizi ni kipengele cha Isimu ambacho hushughulikia matumizi sahihi na sanifu ya lugha.
7. Tazama jarida la Letters to Editors and Tributes (1987) ambalo mhariri wake ni Dumila Faraj uk. 30.

SURA YA NNE

4.0 MAONI NA MAPENDEKEZO KUHUSU UKUZAJI NA
NA UENDELEZAJI MWEMA WA KISWAHILI

4.1 UTANGULIZI

Maoni yangu ni kwamba Kiswahili kinaweza kuunda maneno yote yanayohitajika kutajia yote kinachotaka katika nyanja zote.¹
(Tasiri Yetu).

Haya maoni yana maana kwamba Kiswahili hakijitoshelezi katika nyanja zote na kwa hivyo kuna haja ya kuunda maneno ili kujaza pengo hili. Langacker, R. W. katika kitabu na ukurasa tuliokwisha nukuu hapo nyuma asema kuwa kila lahaja (au lugha) hujitosheleza na pale ambapo haijitoshelezi hufanya kila njia ijitosheleze. Hivi ndivyo kilivyo Kiswahili pia maana kina utaratibu wake wa kujitosheleza kulingana na hali na wakati.

Lengo la sura hii ni kutoa maoni pamoja na mapendekezo kuhusu ni vipi ambavyo Kiswahili kinaweza kukuzwa vema ili kikubalike kote kinakozungumzwa. Aidha, sura hii itatoa maoni kuhusu yanayopaswa kufanywa ili kukipa Kiswahili nguvu kama lugha ya kimataifa licha ya kuzungumzia umuhimu wa kukikuza Kiswahili kwa jumla.

4.2 UKUZAJI WA KISWAHILI KULINGANA NA ULIMWENGU WA SASA

Lugha kama chombo cha mawasiliano yapaswa kukuzwa ili kutekeleza wajibu wake ipasavyo. Lugha ambayo haikui hupungukiwa na msamiati na vile vile istilahi. Kuna wataalamu kama Broomfield na Lyndon Harris waliodai kuwa Kiswahili hakijitoshelezi maana lazima kikope kutoka kwa Kiarabu. Madai haya ni ya kuzua tu maana hayana msingi katika uzingatifu wa isimu ya lugha. Tunavyojua ni kwamba kila lugha ni lazima ijitosheleze kulingana na matakwa ya wanayoizungumza. Endapo kutakuwa na upungufu kuna njia mbalimbali za kutumiwa ili kuhakikisha kwamba upungufu huo umeondolewa.

Kumekuwa na njia mbalimbali za kukuzia Kiswahili. Njia hizi zimekuwa nzuri ijapokuwa hazina utaratibu maalumu. Sisi tungependa kuchukua msimamo huu: Kiswahili ni lugha na ikiwa haina msamiati wa kutajia kifaa fulani jambo la kwanza la kufanya ni kutafuta na kubukua katika lahaja zote za lugha hii maana tukichunguza lahaja za lugha hii tunaweza kusema kuwa Kiswahili si kimoja. Basi, ikiwa, kwa bahati nzuri, mojawapo ya lahaja za Kiswahili ina neno la kutajia kifaa hicho, na lichukuliwe mara moja. Ni kwa kufuata njia hii, ndiyo Kiswahili Sanifu kikapata

istilahi 'Kisabeho' kutoka kwa Kipemba kwa maana ya 'Breakfast dish', yaani kifungua-kinywa lakini kisicho cha majimaji.

Ikiwa lahaja za Kiswahili hazina masamiati unaotafutwa itatubidi tukope. Maoni ya baadhi ya wasomi na wataalamu ni kuwa ikiwa lahaja za Kiswahili hazina msamiati tunaotaka basi tukope kutoka kwa lugha za Kibantu.² Halafu hatua ya tatu inayopendekezwa ni kuwa tukope kutoka kwa lugha za Kiafrika pale ambapo lugha za Kibantu zimeshindwa kutupa msamiati mwafaka unaotafutwa. Mwisho kabisa, kuhusu ukopaji, eti hatua hizi zote zikishindwa ndio twende kokote kule.

Sisi maoni yetu ni tofauti: Shughuli yetu kubwa ni kukopa bali si wapi pa kukopa. Twasema hivi maana ukopaji na wapi pa kukopa hutegemea ni msamiati gani unaotakikana. Kwa mfano, hukuna haja kutafuta kisawe cha neno la Kiingereza 'Missile' katika lahaja za Kiswahili, lugha za Kibantu au zile za Kiafrika kwa jumla. Tunalosema ni kwamba njia hizi zote ni nzuri lakin lazima tuwe na mantiki katika kuzitumia. Yaani, sharti tujue tunazitumia kwa nani, wapi, vipi, lini na kwa sababu gani.

Mbali na haya tunayoyasema kuhusu ukopaji, katika kuifanya shughuli hii lazima tuwe na tahadhari.

Daima ikumbukwe kuwa katika kukopa lazima tuyakope maneno ambayo yanaweza kukubalika katika Kiswahili (Lugha pokezi) maana maneno kama 'Lweya' kutoka katika Kinyamwezi kwa maana ya 'Virgin Land' na 'Lusoko' kutoka katika Kisukuma kwa maana ya 'Caldera' ijapokuwa yamekopwa kutoka lugha za Kibantu na kuingizwa katika Kiswahili yatabaki tu katika makamusi na vitabu vya wasomi maana haya ni maneno ambayo kwa maoni yetu, yamelazimishwa na wasomi katika Kiswahili ilhahi hayana ule mwonjo wa maneno ya Kiswahili. Hapa tuna maana kuwa katika kukopa hatukopi lugha bali twakopa dhana na kwa hivyo baada ya kukopa lazima tukirekebishe kile tulichokikopa ili kiingie sawasawa katika mfumo wa lugha pokezi, isipokuwa pale ambapo lugha changizi na lugha pokezi zina miundo inayofanana kabisa.

Ingawa kukopa husaidia kuikuza na kuipanua lugha, kama anavyosema Besha, R (1972:23) siyo lazima lugha ichukue maneno ya kigeni kila mara kunapokuwa na jambo jipya la kueleza. Maneno ya lugha inayohusika (lugha pokezi) yanaweza kupanuliwa maana zake mpaka yakaeleza mawazo hayo mapya au kutoa maana maalumu kwa maneno ya kawaida. Kwa mfano, maneno 'Munyu' na 'Chumvi' ni maneno yenye maana inayoingiliana lakini kumekuwa na rai kutoka kwa Wanataasisi kuwa 'Chumvi' litumike kwa maana ya 'Salt' nalo 'Munyu' litumike kwa maana ya 'Sodium Chloride'. Endapo

rai hii itakubalika basi maneno haya mawili: Chumvi na munyu yatakuwa yamepanuliwa maana zake na kueleza dhana mpya ya 'Sodium Chloride'.

Isitoshe, badala ya kukimbilia kukopa, baadhi ya dhana na vifaa vipya katika kiswahili vipewe majina kutokana na utendakazi wake. Kwa mfano, ikiwa kumekuja kifaa ambacho kazi yake ni kulevya kikiitwa kileo itafaa zaidi kuliko kwenda kukopa maana ukopaji huichafua lugha kwa kuiletea miundo mipya. Mfano mwingine wahuu 'Motorcycle'. Kilipokuja kifaa hiki Waswahili hawakuwa na jina la kukitajia lakini kutokana na mwendo wake wa tu tu tu tu kikaitwa Kitututu au Piki piki na likashika.

Kiswahili, kama zilivyo lugha nyingine za Kibantu, kina bahati ya kuwa na uwezo wa kunyumbuka na kwa hivyo kutokana na mzizi wa kitenzi kimoja kuweza kuunda maneno mengine. Kwa mfano, kutokana na sifa zifuatazo tuna maneno haya:

Bora -----Boresha

Maskini ---Maskinisha, Maskinika n.k.

Shinda ---- Mshindi, Mshindwa, Mshinde n.k.

Kiswahili pia kinaweza kuunganisha maneno mawili au zaidi ya kawaida ili kuunda neno moja litakalotoa maana mpya. Kwa mfano, Meno + Mbwa → Menombwa kwa

maana ya 'Incissors' ambayo ni meno yanayofanana na meno ya mbwa.

Utohozi ni moja katika njia maarufu sana za ukuzaji na upanuaji wa Kiswahili. Utohozi ni namna ya kuunda majina hivi kwamba maneno ya lugha changizi yanafuata muundo wa lugha pokezi. Utohozi pia ni kuunda maneno kwa kuchukua sehemu fulani za maelezo. Katika utohozi huingizwa akronimu³ pamoja na kaleki⁴ ambazo baadhi ya wataalamu wameita 'tafsiri kopa'. Mifano ya maneno yaliyoundwa kutokana nautohozi ni ifuatayo: CHAJIO kutokana na Chakula cha Jioni, FUPAJA kutokana na Mfupa wa Paja, UKIMWI kutokana na Upungufu wa Kinga Mwilini, DC au DISII kutokana na D.C. la Kiingereza, PC au PISII kutokana na P.C. la ~~Kiingereza~~, Baba Sukari⁵ kutokana na Sugar Daddy la ~~Kiingereza~~ na Kemia kutokana na Chemistry la Kiingereza.

Ijapokuwa utaratibu huu wa utohozi unasaidia sana katika kukikuza na kukiendeleza Kiswahili, kigezo cha utohozi huu hakijulikani. Kwa mfano, kwa nini Fupaja lisiwe Mfupaja, au kwa nini Chajio lisiwe Chajioni? Ili utohozi katika Kiswahili upate kukubalika lazima ushirikishe vikao vya watu wenye ujuzi wa Lugha na Isimu. Na wataalamu hawa sharti kuhakikisha kuwa msamiati matokeo ni wa lugha nyepesi na una msamiati mwenza katika Kiswahili ambayo ni lugha pokezi.

Lugha hapanuliwa kila uchao ili iweze kukidhi mahitaji ya watumiaji wake. Hali hii huwa na athari mbili kwa lugha ile inayohusika: kuiongezea msamiati, na kuiletea lugha pokezi miundo mipya ya maneno. Basi ni jukumu la watumiaji wa lugha fulani kujitokeza na msamiati unaofaa zaidi pale unapohitajika na kitendo hiki kitafanikiwa zaidi ikiwa juhudi hizi hazitakuwa za kasi sana na pia ikiwa hazitaachiwa watu wachache katika jamii ya wazungumzaji wa lugha hiyo.

4.3 YANAYOPASWA KUFANYWA ILI KISWAHILI KIKUZWE KOTE KAMA LUGHA MOJA

Ili lugha ya Kiswahili kikuzwa vema sharti pawe na ushirikiano baina ya wakuzaji maana kitu chochote kifanywacho kwa hisia za ubinafsi huwa hakina misingi madhubuti na kwa hivyo si mno kudumu. Yaani, katika kutayarisha istilahi za Kiswahili haja inapojitokeza watu mbali mbali lazima washirikishwe. Na watu hawa isiwe ni kila mtu aijuaye lugha hii bali pawe na mantiki na busara katika kuwashirikisha. Ushirikiano huu uwe wa wafuatao: - Kwanza, mabingwa na wataalamu katika nyanja inayoshughulikiwa. Kwa mfano, ikiwa ni nyanja ya uhandisi inayoshughulikiwa wataalamu katika nyanja hii wafaa sana. Pili, wataalamu katika lugha na isimu ya Kiswahili lazima washirikishwe ili kutoa mwanga kuhusiana na muundo wa Kiswahili

ili lugha hii isije ikapewa muundo ambao si wa Kiswahili, hali ambayo inaweza kuleta matatizo katika kutamkwa kwa zile istilahi ambazo zitakuwa zimeundwa. Halafu tusiwasahau 'Waswahili wenyewe' wakiwa ni watu ambao ni watumiaji wa Kiswahili kama lugha iliyo wazaa na kuwalea. Lakini ikiwezekana Waswahili ambao wafanya kazi katika nyanja mbalimbali waulizwe kuhusu misamiati ya nyanja hizo katika Kiswahili. Inapolazimu Waswahili washirikishwe, kwa kukosa Mswahili katika nyanja fulani, ikumbukwe kuwa kwa sababu ya wingi wa lahaja Kiswahili si kimoja. Basi itakuwa vema ikiwa karibu kila lahaja ya Kiswahili itashirikishwa maana kuna uwezekano wa lahaja fulani kuwa ina jina la kutajia kifaa fulani huku lahaja nyingine hazina. Basi kutoshirikishwa kwa wazungu-mzaji wa lahaja kama hii kwaweza kuwafanya walioko katika mkutano fulani kukata kauli kwamba Kiswahili hakina jina la kutajia kifaa hicho kumbe lipo. Halafu ikiwezekana watu wa marika mbalimbali pia washirikishwe. Kwa mfano, katika uundaji wa istilahi za Kijamii ikumbukwe kuwa jinsi mzee anavyoitumia lugha si sawa na anavyoitumia mtu wa makamo au kijana. Yaani, kuna uwezekano wataalamu ambao ni watu wa makamo wakapendekeza neno fulani litumike kama istilahi ya kifaa fulani lakini kwa kulisikia tu wazee wakacheka au wakanuna.

Kabla ya kukata shauri kuwa neno fulani liwe ndilo istilahi ya jambo fulani lazima pawe na majadiliano baina ya washiriki, ambao kwa maoni yetu lazima wawe wametoka karibu kila pembe kunakoongewa Kiswahili. Hapa tuna maana kwamba katika kupata istilahi fulani pawe na mjadala ambao hauna bundi kuwa na vigezo. Vigezo hivi kila mara vijikite katika misingi ya ISO ili Kiswahili kikuzwe kama lugha ya kimat-aifa. Hata hivyo, istilahi zipatikanazo hivi lazima zipururwe ili kuzitoa ugeni kusudi zipate kuingiliana na mfumo na muundo wa Kiswahili. Pia, orthografia na matam-shi ya Kiswahili hayana budi kuzingatiwa.

Nyingi ya warsha na semina ambazo zimeshughulikia ukuzaji wa Kiswahili zimedhaminiwa na UNESCO. Wapenzi wa Kiswahili kote ulimwenguni hawana budi kulionyesha shirika hili kuwa wanazitambua fadhila hizi kwa kulipa shukrani. Lakini shukrani pekee hazitoshi. Lazima hawa wapenzi wa Kiswahili washirikiane na UNESCO, kwa mfano kwa kuhudhuria semina kama hizi kwa wingi ili kulionyesha shirika hili kuwa kweli wao ni wapenzi wa Kiswahili na kuwa wanazitambua juhudi za UNESCO. Hivi, shirika hili likiombwa kuzidi kutayarisha vikao vya aina hii vinavyowawezesha wanalugha kuja pamoja litakuwa radhi kufanya hivyo. Si hivi tu bali mashirika mengine yanayoweza kugharamia vikao vya aina hii kama vile SIDA, OAU, n.k. yaombwe kusaidia katika

harakati za kuandaa semina kama hizi ili isije ikaonekana kama kwamba wapenzi wa Kiswahili wametosheka na huduma zinazotolewa na UNESCO kiasi kwamba hawahitaji msaada mwingine wowote kutoka kwingineko. Pia, serikali za mataifa ya Afrika Mashariki na ya Kati ambako Kiswahili ni lingua franca kwingi hazina budi kuzisaidia juhudi za kuikuza lugha hii. Kisha makampuni mbalimbali nchini pamoja na watu matajiri waweza kusaidia katika ukuzaji wa Kiswahili kwa kutoa michango ya kifedha, ikiwa wataelezwa umuhimu wa kuikuza lugha hii.

Baada ya kutayarisha istilahi, huo usiwe ndio mwisho wake. Lazima istilahi hizo zisambazwe kote Kiswahili kinakotumiwa ili kuingizwa katika mkondo wa watumiaji wa lugha hii mara moja. Istilahi hizo sanifu zitumiwe katika vyombo vya mawasiliano kama vile katika redio, magazeti, sahani za santuri, televisheni na pia kwa kutumiwa na walimu na wanafunzi mashuleni, wachapishaji wa vitabu, na watu mashuhuri katika jamii mathalani wabunge katika kuuongelea umma. Hivi istilahi zilizosanifishwa zitashika kwa kasi kuliko pale zinapohifadhiwa katika makamusi maana tajriba yetu kama wasomi imetufanya kukata kauli kuwa ni watu wachache sana katika jamii walio na makamusi na pia wayatumiayo kwa kuukuzia ujuzi wao wa lugha.

Baraza la Kiswahili la Taifa, Tanzania
(BAKITA) linafanya kazi kubwa katika ukuzaji wa Kiswahili. Ni fikira zetu kwamba ikiwa nchi nyingine za Afrika Mashariki na Kati sitakuwa na mabaraza kama BAKITA, Kiswahili kitapiga hatua kubwa sana kimaendeleo kama lugha ya kimataifa. Labda kutokuweko kwa mabaraza haya kwatokana na hofu kuwa yatafanya kazi moja. Pendekezo letu ni kwamba kuwe pia na Baraza la Kiswahili la Bara la Afrika ambalo litatoa kauli ya mwisho kuhusu istilahi zitakazopendekezwa na mabaraza haya madogo yatakayopatikana kwa kiwango cha kitaifa. Ili mabaraza haya yafanye kazi vizuri, itafaa zaidi ikiwa mafunzo yanayohusiana na leksikografia au msamiati yataanzishwa. Kisha kuwe na kozi za namna ya kukusanya maneno ya kusanifishwa. Hili likifanyika kutakuwa na hazina au benki ya msamiati ambayo itaendewa kila mara unapohitajika msamiati wa nyanja fulani. Halafu ili kuendeleza juhudi hizi kuanzishwe jarida la kutoa msamiati sanifu. Jarida hili lingelitwa KISWAHILI: MSAMIATI SANIFU.

Katika kuhitumisha, na ikumbukwe kuwa kazi ya uundaji wa istilahi katika lugha yoyote ile haina mapumziko kwa kuwa lugha huhitaji kupanuliwa kila uchao kusudi iweze kukabiliana kikamilifu na mambo mapya yazukayo katika jamii. Basi baada ya warsha fulani kuhusu Kiswahili kwisha, swali daima liwe

ni: Je, ni lini kutakapokuwa na warsha nyingine ya kushughulikia lugha hii ili kusiwe na hali ya kusangaa katika kuiendeleza? Na ili istilahi zilizoundwa zipate kukubalika lazima wale walioziunda waushawishi umma kuwa wanafanya kazi nzuri maana umma ndi mkubwa katika ukuzaji wa lugha.

4.4 UMUHIMU WA KUKIKUZA KISWAHILI

Dhana ya ukuzaji wa lugha na maana ya hatua zinazoweza kuchukuliwa ili lugha fulani iweze kutumiwa na watu wengi zaidi na pia lugha hiyo iweze kuwa dhabiti kimasamiati.⁶ Licha ya lugha inayokuzwa kuzungumzwa na watu wengi, Maganga, C. (1983:93) asema kuwa watu hao hawana budi kuihusisha lugha hiyo katika shughuli zao mbalimbali za kila siku. Lugha ya Kiswahili ni Lugha ya Taifa katika mataifa mengi ya Afrika Mashariki na Kati. Basi kuna haja ya kuikuza lugha hii ili watumiaji wake wajihisi wana chombo madhubuti cha mawasiliano na hivi watakitumia katika shughuli zao za kila siku.

Kitumbo, W.H.L. (1959:227-8) asema kuwa lugha ya Kiswahili yazungumzwa kwingi barani Afrika lakini Kasoro yake ni kwamba kila mzungumzaji anaizungumza kivyake. Kwa sababu hii kuna haja ya kuikuza lugha hii katika mwelekeo mmoja ili Kiswahili kijitokeze

kama lugha moja na wala si vilugha, hali ambayo yavuruga mawasiliano baina ya wazungumzaji wa Kiswahili.

Inafikiriwa kuwa bara la Afrika ndilo lililo na lugha nyingi zaidi ikilinganishwa na mabara mengine ulimwenguni. Isitoshe, ni bara la Afrika tu lililogawanywa kufuatana na lugha za wageni waliolitawala kama wakoloni. Hali hii imeifanya Afrika kujulikana kufuatana na maeneo kusemwapo Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu na Kireno.⁷ Migawanyiko hii ni kifaa cha kuwatenga Waafrika wenyewe kwa wenyewe ili wajihisi na kujiona kuwa ni tofauti na wenzao kwa sababu ya tofauti za lugha. Hali hii haina budi kurekebishwa na hili litawezekana tu ikiwa Waafrika watatanabahishwa kwamba kuna kifaa cha utamaduni wa Kiafrika kinachoweza kuwaunga pamoja (Mazrui, A. na Tidy, M. 1984:299).

Ingawa lugha ya Kiswahili imekuwa ikitumiwa kwa muda mrefu sana kama chombo muhimu cha mawasiliano kati ya watu wa bara hili mathalani katika biashara ya watu mwa Afrika Mashariki na Kati, tokea kupatikana uhuru Waafrika wengi hawajaonyesha kuwa lugha hii yastahili kukuzwa au kuendelezwa ili iendeleo kutekeleza jukumu lile la siku za nyuma. Hata hivyo, umuhimu wa lugha hii katika Afrika na hata nje yake unaendelea kujidhirisha wazi. Kutokea siku za ukoloni wa Mzungu Kiswahili kimekuwa kikifunzwa katika shule za Afrika Mashariki na hata kwingineko ulimwenguni. Umaarufu wake

unajidhihirisha zaidi kwa kufanzwa kwake kama somo la lazima katika shule za msingi na za sekondari nchini Kenya katika mfumo mpya wa elimu ya 8:4:4:, kufunzwa katika vyuo na taasisi nyingi ulimwenguni, kufunziwa masomo mengine katika shule za msingi na pia somo la siasa katika shule za sekondari nchini Tanzania, kufunziwa katika madarasa ya chini ya shule za msingi mashariki mwa Zaire, na kutangazwa kwake katika idhaa nyingi za redio.

Harakati hizi zote zaonyesha jinsi lugha ya Kiswahili ilivyo maarufu na hili laungwa mkono na Gibbe, A.G. (1983:50) anayesema kuwa Kiswahili kimewavutia wasomi wengi duniani kote kiasi kwamba mwanzoni mwa miaka ya 1970 baadhi ya waandishi wenye vipawa vya hali ya juu kutoka Afrika Magharibi akiwemo yule mwandishi maarufu Wole Soyinka walisema kwamba yafaa Kiswahili kiwe lugha ya usomi barani Afrika, hii ikiwa ni hatua ya kuifanya lingua franka ya bara la Afrika. Maoni haya hayakukomea hapo kwani hivi majuzi Wole Soyinka alipokuwa akikabidhiwa tuzo la uandishi bora alisisitiza haja ya kuwa na Kiswahili kama lingua franka ya bara zima la Afrika.

Bila shaka Soyinka kama mwandishi aliyeandika kwa muda mrefu na kwa lugha ya kigeni, isiyo ya Kiafrika,

anafahamu kuwa kuna mambo au hisia fulani ambazo Waafrika wanaweza kuzizungumzia vema zaidi katika lugha ya Kiafrika kuliko wanavyoweza kufanya katika lugha ya 'wenyewe'. Kiswahili ni lugha ya Kiafrika na ni lugha ambayo imeikiuka mipaka ya ukabila au utaifa. Kwa sababu hii, hii ni lugha ambayo kila Mwafrika mwenye busara sharti kuikubali. Lakini ili kuikubali, lugha ya Kiswahili lazima ijitokeze kama lugha moja na yenye misingi imara. Hili litawezekana tu ikiwa lugha ya Kiswahili itafanyiwa juhudi za lazima za kukuzwa ili watumiaji wake wapate kitu cha kujivunia kimawasiliano.

4.5 HITIMISHO

Katika kuishughulikia mada yetu ya utafiti, nia yetu imekuwa ni kueleza jinsi ambavyo Kiswahili chaweza kukuzwa kama lugha ya kisasa na kujadili juhudi zilizofanywa katika kukikuzwa na kukiimarisha Kiswahili baada ya kupatikana kwa uhuru katika Afrika Mashariki. Isitoshe, lengo letu limekuwa ni kuunga mkono au kupinga rai kuwa tofauti ipatikanayo katika Afrika Mashariki kilugha yatokana na hali ya kila nchi kurithi sera tofauti ya lugha kutoka kwa wakoloni wa Kizungu. Masuala ya kwanza mawili yameshughulikiwa waziwazi. Ijapokuwa suala la tatu limeshughulikiwa, msomaji ameachiwa uhuru wa kukata kauli ni mkondo upi wenye uzito, yaani

ni kweli au la. Hata hivyo, kwetu, kuweco kwa hali tofauti kilugha katika Afrika Mashariki kwasababishwa na masiala kadhaa. Kwanza ni kuweco kwa viongozi katika baadhi ya nchi ambao ni walezi imara wa Kiswahili kinyume na wale walio katika nchi nyingine. Rais wa Tanzania aliyeng'atuka Mwalimu Julius Nyerere akiwa mtunzi wa vitabu ni mfano wa mlezi imara wa Kiswahili. Naye Milton Obote, aliyekuwa wakati mmoja raisi wa Uganda, ni mfano wa kiongozi asiye mlezi wa Kiswahili maana

Wakati wa uongozi wa Rais Milton Obote Kiswahili hakikutambuliwa kama lugha rasmi. Lugha za kwanza zilitumiwa katika shule za msingi. Kufika darasa la nne na la tano Kiingereza kilitumiwa kama lugha ya mafunzo. Kila wizara ilikuwa na msimamo wake kuhusu lugha ...⁸

Jambo la pili liletalo tofauti kilugha katika Afrika Mashariki ni hali ya kutokuwa na sera za lugha zinazofanana. Yaani inakuwa ni kila nchi kujitahidi kivyake na katika mwelekeo wake. Suala hili, kidogo, laingiliana na lile la kwanza. Halafu suala la tatu linalosababisha kuweco kwa hali tofauti kilugha katika mataifa ya Afrika Mashariki lafungamana na historia ya nchi hizi kwa jumla. Tukitazama hali ya Kiswahili nchini Tanzania kihistoria twaona kuwa nchi hii (hasa Tanganyika ya wakati huo) iliwahi kutawaliwa na Wajerumani. Wajerumani hawa hawakutaka Waafrika, ambao kwao walikuwa washenzi, waifahamu lugha yao tukufu

ya Kijerumani. Pia kutotaka Kijerumani kijulikane na Waafrika kulitokana na kuchelea siri zao zisije zikajulikana na watawaliwa. Basi walihimiza matumizi ya Kiswahili, lugha ambayo ilikuwa ikifahamika kwingi Tanganyika, badala ya Kijerumani. Walipokuja Waingereza kuitawala nchi hii walikikuta Kiswahili na misingi imara na kwa hivyo wakalazimishwa na hali hii kukiendeleza mpaka pale nchi hii ilipojipatia uhuru. Pia, kihistoria, watu wengi wa Afrika Mashariki walifanywa na Waingereza kukiabudu Kiingereza kuwa ndicho kitambulisho cha mtu aliye na elimu ya juu. Kwa mfano mtazame mlevi katika Rosa Mistika cha Kezilahabi anapomwambia Rosa, 'I know English Makerere'. Kwa nini hamwambii yuakifahamu Kiswahili? Waganda nao kihistoria wamekataa kukikubali Kiswahili kwa kuwa katika fikira zao Kiganda ni bora kuliko Kiswahili maana ni lugha yao, lugha ya watawala wa kutoka jadi. Kwa maoni yetu basi kuwa na tofauti kilugha katika Afrika Mashariki hakusababishwi na hali ya kila nchi kurithi sera tofauti ya lugha wakati wa kujipatia uhuru. Kurithi sera tofauti za lugha wakati wa kujipatia uhuru ni sababu changizi tu na kwa hivyo hatuwezi kuichukua kuwa ndiyo iliyosababisha kuweko kwa hali tofauti kilugha katika Afrika Mashariki.

Kuna mambo mengi ambayo yangeweza kuingizwa katika mada hii ya utafiti lakini kwa sababu ya upana wa mada yenyewe tumelazimika kuyaacha nje. Lakini tunatumanini ya kwamba machache tuliyodokeza hapa yatatoa mwanga kuhusiana na ukuzaji wa Kiswahili. Aidha tunategemea kwamba tuliyoyataja hapa yatawachoea moto wasomi wapenzi wa Kiswahili kulishughulikia suala hili kwa upana zaidi. Ni fikira yetu kuwa hili likifanywa upungufu usemwao kuwa Kiswahili kinao utakoma. Lakini baadhi ya yaliyosemwa humu yanaweza kupanuliwa kadiri utakavyotaka wakati.

4.6 TANBIHI

1. Mtazame Temu, C.W. katika Kiswahili Toleo la 42, 1972 chini ya kichwa: Swahili Vocabulary Expansion: A Preliminary Observation.
2. Wasanifishaji wa Kiswahili mnamo mwaka 1930 walikuwa na mawazo kama haya. Isitoshe, Abdallah Barua alipokuwa akihojiwa na Mwalimu Kazungu Kadenge kuhusu Kiswahili kikuzweje katika kipindi cha Sauti ya Kenya Redio kiitwacho Ukumbi wa Kiswahili alikuwa na maoni kama haya.
3. Akronimu ni jina linalotokana na ufupisho wa maneno kwa kutumia herufi za mwanzo kama inavyoonekana katika mifano iliyotolewa.
4. Kaleki ni ama ukopaji wa mofimu kwa maana yake, au tafsiri ya mofimu kwa mofimu, kwa mfano D.C. kuwa Disii (au DC), au Sugar daddy kuwa Baba sukari.
5. Ingawa tumetoa Babasukari kama mfano wa utaratibu wa utohozi, neno hili halijashika sana katika Kiswahili Sanifu. Haikosi juhudi za kulipata zilikuwa za kasi sana.
6. Neno 'msamiati' limetumiwa hapa likiwa na maana ya neno lolote lipatikanalo katika lugha fulani

na wala si kama watu wengine wanavy^ofikiria kuwa neno
'msamiati' lina maana ya neno gumu lisiloeleweka
katika lugha fulani.

Je kigezo cha neno gumu ni kipi?

7. Mtazame Kihore, Y.M. katika MULIKA Na. 15 chini
ya kichwa: Nafasi ya Kiswahili Barani Afrika.
8. Mbaabu, I katika Kiswahili: Lugha ya Taifa
uk. 6.

MAREJEO

- Akida, H. (1983): Ukužaji na Uendelezaji wa Msamiati wa Kiswahili. Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili I, TUKI, Dar es Salaam
- Allen, J.W.T. (1959): Rapid Spread of Swahili. Swahili Vol.30, Makerere College Library (Wachapishaji)
- Andrzejewski, B.W. (1971): The Role of Broadcasting in Adaptation of the Somali Language to Modern Needs. - Language and Social Change. Whiteley, W. H. (Mhariri). OUP, London.
- Baraza: Gazeti la Kiswahili, Kenya Tarehe 9 Mei 1974.
- Besha, R. (1972): Lugha ya Kiswahili hivi leo: hasa katika Siasa. Kiswahili Vol. 42, Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili, Dar es Salaam.
- _____ (1983): Utayarishaji wa Vitabu vya kufunzia Wageni Kiswahili. Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili II, TUKI, Dar es Salaam.
- Broomfield, L. (1965): Language History from Language

by Leonard Broomfield. Harry Hoijer (Mhariri).

Holt, Rinehart and Winston, Inc.

Bull, A.F. (1961): The Story of the East African Swahili Committee: Looking Back 30 years and Forward. Kiswahili No. 32. East African International Language Swahili. Allen, J.W.T. (Mhariri).

Chiraghdin, S. na Mnyampala, M.E. (1977): Historia ya Kiswahili. OUP, Nairobi

Crystal, D. (1971): Linguistics. Hazel Watson and Vinely Ltd, Great Britain.

DAILY NEWS - Gazeti la Kiingereza, Tanzania.

Tarehe 21 Oktoba, 1987.

Dumila, F (1987): Letters to Editors and Tributes. Nisher Printers Ltd, Mombasa

Fanon, F. (1961): The Wretched of the Earth. Francois Maspe'ro e'diteur 1961.

Fishman, J.A. (Mhariri) (1968): Language Problems of Developing Nations. John Wiley and Son, Inc. U.S.A.

Fulass, H. (1971): Problems of Terminology. Language and Social Change. Whiteley

(Mhariri). OUP, London.

Gibbe, A.G. (1983): Maendeleo ya Istilahi za Kiswahili.
Makala za Semina ya Kimataifa ya
Waandishi wa Kiswahili I, TUKI,
Dar es Salaam.

_____ (1984): Tanzania's Language Policy With
Special Reference to Kiswahili as
an Educational Medium. Kiswahili
Vol. 50/1, TUKI, Dar es Salaam.

Gumpertz, J.J. (1968): Types of Linguistic Communities.
Readings in the Sociology of Languages.
Fishman, J.A. (Mhariri) Mouton and
Co. Printers, The Hague.

Hartmann, R.R.K na Stork F.C. (?): Dictionary of
Language and Linguistics. Applied
Science Publishers Ltd, London.

Kamusi ya Kiswahili Sanifu (1981), TUKI, Chuo Kikuu cha
Dar es Salaam.

Kamusi ya Tiba (Musuada): Idara ya Isimu na Lugha
za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kapinga, M.C. (1983): Sarufi Maumbo ya Kiswahili,
TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

- Khamis, A.M. (1983): Kiswahili Ikiwa ni Lugha ya Kimataifa. Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili I, TUKI, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.
- Khatibu, M.S. (1983): Historia ya Maendeleo ya Kiswahili Zanzibar. Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili I, TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Kihore, Y. M. (?): Nafasi ya Kiswahili Barani Afrika. Mulika Na. 15, Jarida la Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam. Masoko, D.L.W. na Mdee, J.S. (Wahariri)
- Kitumbo, H.W.L. (1959): Kiswahili Usages, Congo Belge and Ruanda Urundi. Swahili Vol. 31. Makerere College Library (Wachapishaji) Allen, J.W.T. (Mhariri)
- Krapf, J.L. (1982): A Dictionary of the Swahili Language. Tubner and Co. London.
- Langacker, R.W. (1968) :Language and Its Structure - Some fundamental Linguistic Concepts Harcourt, Brace and World, Inc. U.S.A.

- Langacker, R.W. : (1972): Fundamentals of Linguistic Analysis. Harcourt, Brace Javanovich, Inc. New York.
- Lema, A. (?): Hotuba ya Ufunguzi wa Semina. Mulika Na. 2 TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kiimbila, J.K. na Lucas, J. R. (Wahariri).
- Lyons, J. (1970): New Horizons in Linguistics. Hazel Watson and Veney Ltd, Aylesbury, Bucks.
- Maganga, C. (1983): Juhudi za Ukuzaji wa Kiswahili Tanzania Bara. Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili I, TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mazrui, A. na Tidy, M. (1984): Reviving African Culture: Language Policy. Nationalism and New States in Africa from About 1935 to the Present. Heinman General Printers Ltd, Nairobi.
- Mbaabu, I. (1978): Kiswahili: Lugha ya Taifa. Kenya Literature Bureau, Nairobi.
- Mbeo, F.E. (1971): Kukua na kuenea kwa Kiswahili katika mkoa wa Tanga. Kiswahili Vol. 41/1. Jarida la Chuo cha Uchunguzi wa

Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es
Salaam, Kiimbila, J.K. (Mhariri)

Mdari, A.D. (1983): Uimarishaji wa Kufunza na kutumia
Kiswahili katika shule za sekondari
(Mkoa wa Nairobi) Nchini Kenya.
Makala za Semina ya Kimataifa ya
Waandishi wa Kiswahili II. TUKI,
Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Mosha, M. (1971): Loan words in Luganda: A search
for Guides in the Adpatation of
African Languages to Modern Conditions.
Language and Social Change. OUP, London.

Mwamko: Jarida la Chama cha Kiswahili cha Chuo Kikuu
Cha Nairobi. Toleo la Pili (1984).

Mwangomango, J.S. (1972): Kiswahili Karne ya 20. Kiswahili
Vol. 42. Jarida la Chuo cha Uchunguzi
wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar
es Salaam.

Nabahani, S.A. (1982): Barua, Maoni, Mapitio, Mashairi
n.k. Kiswahili Vol. 49/2. Jarida
la Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili,
Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam. Mlokozi,
M. (Mhariri).

Nkwera, F.V.M. (1978): Sarufi na Fasihi: Sekondari
na Vyuo. Tanzania Publishing
House, Dar es Salaam.

Rubin, J. na Jernudd, B.H. (1971) (Wahariri): Can
Language be Planned? Heritage
Printers, Inc. U.S.A.

Snoxall, R.A. (1948): Kiswahili Bulletin No. 21
East African Interterritorial Language
Swahili.

Temu, C.W. (1972): Swahili Vocabulary Expansion:
A Preliminary Observation. Kiswahili
Vol. 42. Chuo cha Uchunguzi wa
Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es
Salaam.

Warsha za Kanda za Kuandaa, Kusanifisha, na Kusabaza
Istilahi za Fizikia, Kemia, Biolojia
na Lugha na Isimu (Novemba 1986
na Aprili/Mei 1987). Chuo cha
Uchunguzi wa Kiswahili, Dar es
Salaam.

Whiteley, W.H. (1969) Swahili: The Rise of a National
Language. Methuen and Co. Ltd. UK.

Wright, M. (1965): Swahili Language Policy. Kiswahili
Vol. 35. Journal of the Institute
of Swahili Research, University
College, Dar es Salaam. Whiteley,
W. H. (Mhariri).